Nipashe
Jumamosi Julai 15, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581372
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

**Kikwete** afichua hujuma kwenye dawa za ARV

UKURASA 5



RIPOTI MAALUM:
**Biashara** mkaa ilivyogeuka vita ya 'paka na panya'

UKURASA 4




UKURASA 11

SAKATA LA BANDARI:

# Samia atema cheche

## • Ashangaa kukithiri malumbano kila uchao, Mbarawa: Ukweli ni huu.... *Ukurasa 2, 3 & 8*



Rais Samia Suluhu Hassan akimwapisha Prof. Kitila Mkumbo kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwenye hafla iliyofanyika Ikulu, Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Wakili Nshala asalimu amri, kukutana uso kwa uso na DCI

UKURASA 3



## ...Mbowe asema ni ajenda ya mikutano CHADEMA kila kona

UKURASA 2

**MICHEZO** **NGOMA RASMI MALI YA SIMBA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6




Aliyekuwa Meneja Masoko na Usambazaji wa Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL) inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Emmanuel Lyimo (katikati), akikata keki wakati wa hafla ya kumuaga ofisi za TGL, Mikocheni, Dar es Salaam jana. Wengine ni Meneja mpya wa Masoko na Usambazaji wa TGL, Dennis Ntaita (kushoto), Meneja Rasilimali Watu, Emmanuel Matondo (wa pili kushoto), Meneja wa Fedha, Samuel Orgeness (wa pili kulia) na Ofisa Utawala, Rehema Shadrack. **PICHA: CARLOS BANDA**

# Samia atema cheche kuhusu Bandari

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amezungumzia suala la uendelezaji wa Bandari ya Dar es Salaam na kueleza kushangazwa na malumbano yanayoendelea siku hadi siku kuhusu suala hilo.

Amesema wakati malumbano hayo yakizidi kuibuka na kuota mizizi, nchi jirani imekimbilia kule kule kusaka fursa, kwa maana ya kutafuta wawekezaji katika bandari yake.

"Lile lile jumba lililowekwa bendera ya Tanzania, limewekwa bendera ya nchi jirani, baada ya kuona malumbano na wao kuona fursa na kuikimbilia ili kuwahi nafasi," alisema Rais Samia jana Ikulu, Dar es Salaam wakati akiwaapisha wateule wake aliowateua hivi karibuni.

"Ninataka kusema vizuri hili suala la fursa na watu wanavyozitumia. Ndugu zangu wakati sisi tunalumbana, tunalumbana bandari apewe nani? Iende isiende, ikae, ivue, isivue, wenzetu kwa kuona malumbano yetu mmeona, wameruka na kwenda kule kule.

"Lile jumba lililowekwa bendera ya Tanzania, limewekwa bendera ya jirani. Sasa Tanzania tumeuza, wale jirani wamekimbilia kule kufanya nini? Na siku ambayo Bunge lilisema kwamba ni ruksa bandari iendeshwe na serikali na sekta binafsi, siku ya pili wenzetu wakasema ninyi ni moja, sisi ni zote zilizoko huku ziende sekta binafsi na wakakimbia kule kwenda kuwahi nafasi kama wale wanalumbana njooni huku.

"Muone jinsi fursa zinavyokuja na kukimbia haraka haraka na jinsi wengine wanavyoweza kuzitumia haraka haraka. Nilisema nitoe mfano huo kuona changamoto na jinsi ya kupata fursa na kuzitumia na kuzifanya zisiponyoke.

"Hilo ni moja lakini amezungumzia hapa (Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango) suala la kubadilisha mwelekeo wa nchi. Hapa pana kazi kubwa kwelikweli lakini niwaombe kwenye nia safi na kwenye nia ya kujenga nchi yetu, msiogope kuja na mawazo ya kubadilisha mwelekeo wa nchi kwa sababu kila mabadiliko yana ugumu wake," alisema.

Rais Samia alisema hakuna mabadiliko rahisi huku akiwakumbusha kuwa, watu wamezoea kushoto na wakiambiwa geuka kulia watalalamika.

**WATEULE**

Rais Samia aliwapongeza viongozi aliowaapisha kwa kuteuliwa lakini akawaambia kazi kubwa ipo mbele yao, hasa kwa mawaziri wawili na manaibu wao.

"Sina la kuwaambia, kazi zenu ni zilezile mmepunguziwa tu mzigo. Nimechomoa mambo kwenu nimemrundikia Kitila Mkumbo (Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji)," alisema.

Alimweleza Waziri Kitila kwamba ana wizara mpya ambayo ndani yake wamo Msajili wa Hazina, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Tume ya Mipango.

"Hii wizara ni muhimu kweli kweli. Kama alivyosema Makamu wa Rais, kama mnaweza kutafuta vichwa vilivyo makini, madhubuti vyenye uzalendo mkavikusanya hapa, basi mkafanye hivyo," alisema.

Rais Samia alitaja sababu ya kuyaweka maeneo hayo matatu ndani ya wizara hiyo kuwa ni sekta zisomane ili litakalotoka hapo liwe limefikiriwa kwenye uwekezaji.

"Liwe limefanyiwa kazi na Msajili wa Hazina ambaye atakuwa ametoa maoni yake anaonaje kwenye mtiririko wa mali na Tume ya Mipango nao watakuwa wameliweka kwenye nafasi yake.

"Litakapotoka hapo yale maneno maneno sasa hili lina kushoto, lina kulia, lina katikati, nadhani yatakuwa hayapo kwa sababu yatakuwa yametoka ndani Wizara ya Mipango na Uwekezaji.

"Kukiwa na uratibu mzuri, muungano mzuri kati yenu. Haya maeneo matatu tunategemea Tanzania yetu itakwenda haraka na itakwenda kwa ufanisi mkubwa na kwa umakini, umakini ndiyo jambo kubwa hatuendi kujaribu na kukosoa, tunakwenda kufanya uamuzi kwa umakini," alisema.

Aliongeza: "Hongera (Kitila) lakini kuna kazi kubwa mbele yako na timu yako Mafuru na wenzio.

Amesema hapa Makamu wa Rais kwamba, mnaweza kuchukua hata nje. Mkisoma kwenye mitandao huko tunakosolewa huko, kushoto, kulia, Kusini, Kaskazini mpaka nje mpaka wapi.

"Wale mnaohisi wana mchango mzuri mnaweza kuwa mkaamua wakaja wakawa sehemu ya tume ya mipango, wakafikiri pamoja na sisi ili tukaondosha lile vuguvugu, wamefikiri nini, wamepanga, tutakuwa tumepanga wote.

"Kila mnayemhisi anaweza kusaidia leteni orodha tuone, tutawafanyia vetting (uchunguzi) vizuri, tuwaweke kwenye tume ya mipango, Tanzania ni yetu wote, wote tufikiri, wote tukawaze kwa ajili ya nchi yetu."

Rais Samia alisema kuna msemo kwamba maendeleo ni suala la haki za binadamu na hayaepukiki, hivyo wanapotaka maendeleo ili Tanzania iendelee lazima wakae, wapange na kufikiri.

"Niwaombe msiende kuona woga wa kufikiri, wala kuja na mapendekezo ambayo ninyi mnaona yataiendesha Tanzania vizuri. Kwenu ni kuwaza na kutuletea, halafu vyombo mbalimbali vitakaa tuangalie, kwa kipindi hiki sisi ndiyo tumepewa dhamana kuleta maendeleo ya Watanzania wote, tufikiri, tuamue, tulete maendeleo," alisema.

Alisema Makamu wa Rais ameeleza hapo kwamba wizara huyo ina changamoto tatu, ikiwamo kuangalia changamoto na fursa hivyo wakaziangalie vizuri.

Mkuu wa Nchi alisema katika suala la mipango mara nyingi nguvu kubwa huelekezwa kwenye rasilimali fedha na kusema kuna suala ambao Tanzania haijafanya vizuri linalohusu maendeleo ya rasilimali watu na kutaka wakaliangalie.

Rais Samia alisema alimteua Katibu Mkuu mapema na kumtaka aanze kujipanga hivyo anaamini kuna vitu ameshavipanga na kwa timu hiyo waende kuchanganya ili kuwe kitu kimoja kinachokwenda vizuri.

"Mwende mkafanikiwe, jicho letu liko kwenu. Kitila una mzigo mzito sasa, kiasi nimeushusha mimi kwangu nimekutwika wewe. Badala ya kuambiwa mama huyu, utaambiwa Kitila huyu, kwa hiyo jiandae kwa hilo," alisema.

## ... Mbowe: Ni ajenda ya CHADEMA kila kona

**Na Beatrice Shayo**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amesema wanatarajia kufanya mkutano ambayo ameiita operesheni katika majimbo 264 itakayokuwa na kaulimbiu ya 'Katiba Mpya Okoa Bandari; kuanzia Julai 28, mwaka huu.

Mbowe aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na maazimio 22 yaliyofanywa na Kamati Kuu ya CHADEMA huku akibainisha kuwa mikutano hiyo itaanzia katika mikoa ya Kanda ya Ziwa na kufuatiwa na Kanda ya Nyasa.

Alisema Kamati Kuu imeazimia mambo mbalimbali ikiwamo kufanya operesheni hiyo kwa nchi nzima kwa ajili ya kuuelezea mkataba huo ili wananchi waufahamu kuwa hauna maslahi kwa nchi.

"Sisi hatuna shida na Dubai. Hoja yetu ni aina ya mkataba ungekuwa na maslahi na nchi tungeingia, barabarani kuipongeza serikali lakini hawataki kufanyia kazi hoja za wananchi katika huo mkataba," alisema.

Mbowe alisema ni vizuri mjadala usikimbizwe na badala yake wachambue yale yote waliyoelezwa na wadau mbalimbali kwa maslahi ya nchi na si vinginevyo.

Alisema wako wanasheria wabobezi wameeleza maboresho ambayo yanatakiwa kufanywa katika mkataba huo, hivyo ni muhimu hoja zao zikafanyiwa kazi.

Aidha, Mbowe alisema Kamati Kuu imeunga mkono kwa jitihada mbalimbali za kupinga mkataba huo ikiwamo waliofungua kesi.

Mbowe alisema hakuna utafiti uliofanywa kuhusu mkataba huo na serikali haijafanya uchambuzi wa kina jambo ambalo haliwezi kukubalika.

"Kamati Kuu imejiridhisha kuwa hakuna ushahidi kwamba serikali ilifanya uchambuzi wa kiuchumi, kijamii, kisiasa au kiusalama kabla ya kuamua na kusaini mkataba huu. Kama hayo yangefanyika na yakawekwa wazi, mjadala juu ya bandari usingekuwa hivi ulivyo," alisema Mbowe.

"Msimamo wetu ni mkataba huo kufutwa tutatumia njia mbalimbali kuhakikisha unafutwa na tunaenda katika operesheni hiyo ya nchi nzima kujenga ushawishi kwa Watanzania tutafanya mikutano zaidi ya 120 na Makamu wangu (Tundu Lissu) na kila kata tutafika," aliongeza.

Alisema wanaunga mkono uwekezaji wenye tija kwa maslahi ya nchi ndiyo maana awali walitoa maoni yao kuhusu uboreshaji wa mkataba huo.

Mbowe alisema Kamati Kuu imeazimia kwamba ikiwa bunge na serikali havitachukua hatua kuhusu malalamiko ya wananchi dhidi ya mkataba wa bandari, chama kitaanzisha na kuhamasisha umma kuchukua hatua kali dhidi ya serikali mpaka itakapousitisha.

"Kamati Kuu imetambua hakuna utafiti wowote wa kisayansi kuonyesha njia mbadala za kuboresha ufanisi wa bandari. Utafiti huo ungesaidia wananchi kulinganisha faida na hasara za kila mbadala unaopendekezwa. Badala yake tumeletewa DP World ikiwa imeshasaini mkataba ili sisi turidhie," alisema Mbowe.



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbalawa, akizungumza katika mkutano na Jukwaa la Wahariri (TEF), kuhusu uwekezaji wa Bandari ya Dar es Salaam jana. Wengine ni Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile (wa pili kushoto), Mkurugenzi wa Sheria wa wizara hiyo, Mohamed Salim (wa pili kulia) na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara, Dk. Ally Possi. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Mbarawa: Ukweli ni huu kuhusu bandari

**Na Jenifer Gilla**

SERIKALI imejibu hoja zilizoibuliwa na watu mbalimbali kuhusu mchakato wa uwekezaji wa Bandari ya Dar es Salaam kati ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) na Kampuni ya DP World ya Dubai, zikiwamo za zabuni ya mkataba huo haikuwa na ushindani.

Hoja nyingine ilikuwa serikali imeiuza bandari zote kwa kuwa utekelezaji huo umefanyika kwa kutumia sheria ya nchi nyingine katika makubaliano hayo.

Katika kujibu hoja hayo, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alisema jana kuwa DP World haijapewa zabuni bila kushindanishwa na kampuni nyingine kama inavyodaiwa, bali imepewa uwekezaji huo baada ya kushinda vigezo vya ubora. Prof. Mbarawa alisema hayo alipokuwa akizungunza na wahariri wa vyombo vya habari jiini Dar es Salaam.

Alisema DP World ilizishinda kampuni zingine zilizoomba zahuni kutoka Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na Ufaransa kwa vigezo vingi ikiwamo uzoefu katika utoaji mizigo bandarini na kuisafirishaji hadi kwa watumiaji.

Waziri alisema aliwema kampuni hiyo pia uwezo mkubwa wa uchangiaji mnyororo mzima wa usafirishaji mizigo, hivyo kuongeza umahiri katika kuihudumia bandari hiyo.

Aidha, alisema mkataba huo ni miongoni mwa mikataba 30 iliyotiwa saini kati ya Serikali ya Tanzania na ya Dubai, wakati wa maonyesho ya kimataifa ya Biashara yaliyofanyika Dubai, (Dubai Expo).

Amesema makubaliano hayo hayana masharti ya kuifunga serikali kuhusu ushirikiano katika utekelezaji wa miradi itakayojadiliwa na kukubaliwa na pande mbili.

Waziri Mbarawa ametaja maeneo ambayo DP World haitakabidhiwa ni gati namba nane hadi 11 katika Bandari ya Dar es Salaam, gati la kupokea mafuta la Kurasini, Bandari za Tanga, Bagamoyo na Mtwara.

Pia alisema mikataba ya utekelezaji itakayoingiwa baadaye itaweka muda wa utekelezaji na marejeo na kwamba uandaaji wa mikataba utafanywa chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) ili kulinda maslahi ya nchi na ajira za wazawa.

**MANUFAA**

Waziri alitaja manufaa ya uwekezaji huo kuwa ni kupunguza muda wa meli kukaa nangani kutoka siku tano mpaka saa 24, kuongeza idadi ya meli zitakazokuja kutoka 1,569 zilizohudumiwa 2022 hadi kufikia 2,950 ifikapo mwaka 2032.

Pia alisema muda wa kushusha makasha (makontena) utapungua kutoka siku tano hado mbili na ushushaji mizigo bandarini kutoka saa 12 hadi saa moja na kwamba gharama za kushusha mizigo zitapungua kutoka Dola za Marekani 12,000 mpaka 6,000 kwa kasha moja kwa mizigo inayokwenda Malawi na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).

"Uwekezaji utaongeza shehena zinazohudumiwa kutoka tani 21.8 hadi 47.57 ifikapo mwka 2032. Mapato ya serikali yataongezeka kutoka Sh. trilioni 7.79 hadi 26.7 ifikapo mwaka 2030 na ajira za Watanzania zitaongezeka hadi zaidi ya 71,000," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Majadiliano ya Mkataba huo, Hamza Johari, alisema hoja kwamba bandari hiyo imeuzwa na kuwa mwekezaji huyo amepewa bandari zote ni upotoshaji.

Alisisitiza kuwa bandari hiyo haijauzwa bali imekodishwa na katika makubaliano hayo kuna vipengele vinavyoelekeza DP World kutositisha mkataba endapo utendaji kazi hautaridhisha.

Johari ambaye ni mwanasheria mbobezi wa mikataba ya kimataifa, alisema suala la mkataba huo halifanyika ghafla bali ni mchakato ulioanzia katika serikali ya awamu ya tano na kufanyiwa upembuzi yakinifu uliyoonyesha kuwa ili serikali ipate matokeo chanya katika uwekezaji wa bandari hiyo, lazima iweke mwekezaji mahiri.

Kuhusu wazawa kukosa ajira, alisema katika Ibara ya 13 ya mkataba inaeleza wazi kuwa lazima mwekezaji aajiri wafanyakazi iliowakuta na itoe kipaumbele kwa kampuni za ndani na kusaidia kujenga vyuo vya mafunzo.

Kuhusu ukomo wa mkataba, Johari ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri Anga Tanzania (TCAA), alisema si kweli kwa kuwa ukomo unawekwa katika mikataba itakayoingiwa ili kuweka misingi.

Kuhusu kutumia sheria ya nchi nyingine katika makubaliano hayo, alifafanua kuwa kwenye sheria za kimataifa mikataba ya baina ya nchi mbili au zaidi inasimamiwa na Mkataba wa Vienna ambao unaelekeza kutumia sheria ya nchi ya tatu katika kutatua migogoro.

Pia alisema mwekezaji huyo hana mamlaka yoyote ya rasilimali zilizoko katika bandari hiyo zaidi ya kupakia na kupakua mizigo inayoingia na kutoka katika meli ili kurahisisha shughuli za bandari.

Kuhusu usiri katika mkataba, alisema mikataba yote ya kibiashara ya kimataifa inapaswa kufanyika kwa siri kwa mujibu wa sheria za kimataifa ili kulinda maslahi ya nchi zilizoingia makubaliano hayo.

# Wakili Nshala asalimu amri, kukutana na DCI

**Na Mary Geofrey**

MAWAKILI wa wakili na aliyekuwa Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Dk. Rugemeleza Nshala, wamesema mteja wao yuko tayari kuitikia wito wa kufika Ofisi ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI).

Mwanasheria huyo alipewa wito na DCI kutakiwa kufika katika ofisi ya Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Kanda Maalum (ZCO) ya Dar Salaam.

Mawakili hao, Nyaroro Kicheere na Jebra Kambole, walisema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati wakizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC).

Walisema mteja wao ana nia njema ya kuitikia wito huo, isipokuwa kwa sasa yuko nje ya nchi (bila kuitaja) na atakaporejea atafika ofisini hapo kutolea ufafanuzi wa kauli zake alizozitoa Julai 3, mwaka huu, kuhusu kupinga Kampuni ya DP World kuwekeza katika Bandari ya Dar es Salaam.

"Rais Mstaafu Dk. Nshala hajakaidi wala kudharau wito huo wa kipolisi na hivi karibuni atarejea nchini na atafika Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam na kutoa ufafanuzi wa yale yote aliyoyasema Julai 3, mwaka huu, kuhusu utata wa bandari," alisema Wakili Kicheere.

"Tunatoa wito kwa vyombo vya ulinzi na usalama hasa Jeshi la Polisi kuhakikisha kwenye sakata hili la mkataba tata wa bandari, Watanzania wote wanapata haki sawa kutoa maoni yao na kama ni wito basi wote wanaokosoa na wanaosifia wapate wito wa kutoa ufafanuzi siyo kwa wakosoaji tu," aliongeza.

Mawakili hao walidai kuwa maofisa ambao ni askari watatu, mmoja aliyevaa kiraia na wawili sare za Jeshi la Polisi, Jumanne ya wiki hii waliingia ofisi binafsi ya mteja wao Wakili Nshala na kufanya upekuzi bila mhusika kuwapo.

"Suala la kuingia ofisini kwa wakili bila kuwapo ni kinyume na Ibara ya 16 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama ilivyofanyiwa marekebisho mara kwa mara ambayo inatoa haki ya faragha," alidai Wakili Kambole,

alidai kuwa walipoingia ofisini hapo askari aliyevaa kiraia alikuwa akimwongelesha msaidizi wa kisheria wa kujitolea wa Dk. Nshala muda wote huku wenzake wawili, mmoja akiingia maktaba bila kusindikizwa wala kuruhusiwa na kushuhudiwa na mtu yeyote au wakili wake na hivyo kutengeneza wasiwasi kama kuna kitu chochote alikiweka au alitoka nacho.

Wakili Kambole alidai wakati hayo yakiendelea askari mwingine alikwenda upande wa pili wa ofisi na kufungua makabati mawili, moja la vitabu na majalada (files) ya wateja wake na kabati lingine la nguo za mahakama jambo ambalo ni kinyume cha sheria.

Mawakili hao walisema kuwa askari hao walifika hapo kwa ajili ya kupeleka wito wa kipolisi uliokuwa unamtaka Dk. Nshala kufika Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi wa makosa ya Jinai, Kanda maalumu ya Dar es Salaam (ZCO) saa 09:00 asubuhi ambayo ilikuwa ni usiku wa manane.

"Kwa hiyo mpaka wito huo unafika ofisini kwake, muda aliopaswa kufika polisi ulikuwa umeshapita," alidai.

Baada ya kauli za wakili huyo kupinga uwekezaji wa bandari na mwekezaji wa DP World, akidai ni kinyume cha sheria na katiba ya nchi kwa kunukuu baadhi ya vifungu vya sheria.

Hivi karibuni wakili huyo alitoka mbele ya vyombo vya habari tena akidai kutishiwa kuuliwa na watu ambao hakuwataja na taarifa hizo alizotoa kwenye vyanzo vyake vya uhakika kutoka serikalini.

RIPOTI MAALUM

# Utafutaji wa mkaa unavyobeba simulizi za 'kufa na kupona' porini

## -Askari-pori, wavunamkaa 'paka na panya'

**Na Frank Monyo, aliyekuwa**
KIBAHA

UNAPOUTAJA Mkoa wa Pwani, ni ulingo uliotawaliwa na utajiri na misitu na maliasili. Lakini, kwa upande wa pili matumizi ya utajiri huo yamebeba ukakasi na madhila mengi.

Madhila hayo yanapotazamwa kwa wajasiriamali wa mkaa, ndilo kundi lenye madhara mengi, vikiwamo vifo, kama anavyosimulia aliyekuwa msafirishaji mkaa, Mohamed Seif:

"Mwaka jana (2022) mwishoni na mwanzoni mwa mwaka huu (2023), nilipoteza rafiki zangu sita kutokana na ajali za pikipiki.

"Mimi pia katika kipindi hicho, nimepata ajali mara sita, nikaona ni heri niachane na hii kazi (kubeba mkaa porini) kwani ninategemewa na familia yangu na ndugu zangu."

Seif, ambaye yuko katika umri wa ujana, mwenye familia ya watoto wawili chini ya miaka 10, mkazi wa Mlandizi, Kitongoji cha Kwala, anamsimulia mwandishi wa habari hizi, kwamba mwishoni mwa mwaka jana alipata ajali zaidi ya sita, zikisababishwa na namna wanavyoendesha pikipiki zilizobeba magunia wastani matatu hadi manne yenye kilo zaidi ya 800.

Hapo Seif, akijutia kutumikia eneo hilo la kutafuta fedha, anataja namna yalivyomkuta ikiwamo mikasa ya kuangukiwa na magunia ya mkaa, akitaja sababu za ajali hizo zinajumuisha wanapokwenda mwendo mkali kuwakimbia askari wa Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) na mara nyingine utelezi mkali unaotokana na mvua, pikipiki inakosa mwelekeo na hata kuwa mwanzo wa ajali inayoendana na mzigo kumwangukia.

"Ukimwona dereva wa pikipiki barabarani amebeba mkaa, ujue ana kilo 800, kwani gunia moja linakuwa na kilo kuanzia 150 hadi 250. Hapo ukikuta dereva akipata ajali kwa kuangukiwa na mzigo, ana hatari kubwa ya kupoteza maisha akichelewa kupatiwa msaada," anasema.

Kijana huyo anasimulia yaliyomkuta katika harakati hizo, ikijumuisha kukohoa damu na kushindwa kupumua vizuri, akifafanua: "Moja ya ajali niliyowahi kupata ambayo ilinisababishia kupumzika kazi hii - tulikuwa tunatoka porini eneo linaloitwa Kimara Misale Kwala (Halmashauri ya Chalinze, wilayani Bagamoyo). Barabara ilikuwa mbovu kutokana na mvua, pikipiki yangu ilinizidi nguvu mzigo wa mkaa ukaniangukia na kunibana kifua.




Mohamed Seif aliyekuwa anasafirisha mkaa kwa pikipiki, akiwa katika biashara yake mpya eneo la Kibamba Chama, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam mwishoni mwa juma lililopita. **PICHA ZOTE: FRANK MONYO**

"Lakini nilipata msaada wa haraka ingawa niliumia sana eneo la kifua na kupelekea kulazwa Hospitali ya Tumbi (Kibaha). Baada ya kukaa hospitalini kwa muda, nikaruhusiwa kurudi nyumbani, maisha yangekuwa magumu, lakini kitu kilichosaidia nilikuwa ninafuga kuku wa kienyeji, nilikuwa ninawauza na kupata fedha pamoja na kitoweo nyumbani."

Seif anasema harakati hizo za kupata mkaa walikuwa wanazifahamu kuwa ni kinyume cha sheria, lakini wazo lao lilitawaliwa na dhana ya 'riziki', wakiendesha nyendo hizo kinyemela porini wakiwa katika kundi la zaidi ya watu 40.

Anasimulia maisha yake ya wakati huo, kwamba kabla ya kuanza safari ya kutoka porini na mzigo, waliwatuma wenzao wanaowaita 'surveyor' kwa maana ya wapelelezi, ambao wakiwahakikishia njia ni salama dhidi ya askari wa TFS, ndipo wanaanza safari kwa makundi, pikipiki zikiendeshwa kwa kasi na mazingira hatarishi kiafya.

Anasimulia chanzo kingine cha ajali ni kuwapo njia mbovu huko wanakofuata mkaa, hasa kipindi cha masika, akiwa na ufafanuzi wake "tunabeba magunia nne, matatu yananyooshwa - yale marefu - na moja linakatwa nusu. Sasa sidhani kama mzigo huo ukikulalia, unaweza kutoka hapo! Ni rahisi sana kupoteza maisha.


"Hivi ninavyoongea kuna jamaa zangu ambao wamenifundisha kazi wameshafariki dunia kutokana na ajali za pikipiki, na ambao tulikuwa kundi moja la watu 40, madereva sita wameshapoteza uhai kwa ajali ya kuangukiwa na mzigo na hiyo ni mwishoni mwa mwaka jana na mwaka huu 2023," Seif anasimulia madhila aliyopitia, akitaja muda wa safari zao ilikuwa kati ya saa saba hadi saa nane usiku, wakiamini hakuna askari wa TFS porini na barabarani.

Katika hilo, Seif na wenzake wanakiuka sheria za nchi. Sera ya Misitu ya Mwaka 1998 na Sheria ya Misitu Sura 323 (marejeo ya mwaka 2002), zinazuia shughuli za uzalishaji mkaa bila kibali na adhabu yake inaambatana na kutaifishwa chombo kinachotumika kusafirisha mazao ya misitu.

### HUJUMA ZILIVYO

Kijana Seif anabainisha kuwa ndani ya mapori ya TFS katika eneo hilo la Mkoa wa Pwani, kuna vijana wanaofanya kazi ya aina yake zaidi ya 3,000 wanaoangamiza misitu kuwa mkaa, wakiishi katika hali ya kinyemela ambayo ni mtihani kwa askari wa TFS kuwabaini.

Anasimulia wakiwa wamejiunda katika staili ya makundi, wanatumia silaha za fimbo za jadi kukabiliana na TFS wanapotokea kutaka kuwadhibiti na mara nyingi wamekuwa wakiwazidi, hata ikawa chanzo cha askari hao wa serikali kutumia silaha za moto na zana za kisasa kwenye vita hivyo.



Moja ya masoko makubwa ya mkaa mkoani Dar es Salaam lililoko Mbezi kwa Msuguri, Manispaa ya Ubungo.

"Ukisikia TFS wanawasaka madereva wa mkaa, wewe utakavyotoka porini huangalii usalama wako, unachoangalia ni mzigo uliobeba, kwa sababu ukikamatwa pikipiki yako inachukuliwa na mzigo unachukuliwa. Kwa hiyo, unakuwa hakuna kitu umefanya. Sasa ili kuepuka hayo yote, unabidi ukimbie hapo ndio ajali hutokea," anasimulia Seif huku huku akisisitiza mali aliyobeba ndio mtaji na tafsiri kuu ya maisha yake.

Seif anamsimulia mwandishi kwamba wanapokuwa porini kusaka mkaa, anakiri kwa kutamka wanakuwa na roho ya kikatili, yenye kumwona yeyote kikwazo kwao, wanaweza kumtoa uhai wake. Anasema kuwa sasa akigeuza uso kukumbuka alikokuwa, ni maisha asiyokubaliana nayo, akirejea mifano na simulizi ya mazito ambayo ni magumu kuwasilisha katika makala haya.

Anaeleza yalivyo mapambano yao barabarani, askari wa TFS huwasubiri kwa kuwavizia na kuna wakati wanachukua hata zaidi ya wiki porini pale wanapopata taarifa za nyendo za wabebaji mkaa ambao safari zao zinakuwa na pikipiki zinazofika 200. Inapotokea mwendeshaji aliyedhurika vibaya au kupoteza maisha, Seif anadai askari wa TFS humwacha mhusika na kuchukua mali zake - pikipiki na mkaa, akitumia mfano wa madai ya kuwapo mkasa wa namna hiyo hivi karibuni eneo jirani na Mto Mondo, Kwala mkoani Pwani.

Anasema katika safari hizo, uhusiano wao na vijana wapelelezi wao, huwa wanachanga fedha kuwalipa kiasi cha Sh. 5,000 kwa kila mmoja kuwafanyia kazi hiyo, Seif akiainisha mbinu za wapelelezi wao:

"Hawa vijana kazi yao ni kuwafuatilia TFS, wakitoa gari tu, wanatupa taarifa na sisi tunaanza kujihami, maana wao wana mtandao mpana wa kujua kila kitu kinachofanywa na TFS dhidi yetu,

"TFS kwa sasa wanapokwenda porini wanafumua matanuri ya kuchomea mkaa," anasimulia Seif na kubainisha mbinu za mapambano hayo ya vikosi vya kiserikali katika kutetea uhai wa misitu.

INAENDELEA UK. 17

## HABARI KITAIFA

# JK aibua hujuma katika dawa za ARV

**Na Waandishi Wetu,** HAI

RAIS mstaafu, Jakaya Kikwete, amefichua siri kuhusu hujuma za udanganyifu zinazofanywa na baadhi ya watu kwa kuweka unga wa muhogo katika dawa feki za kufubaza makali ya virusi vya Ukimwi (ARV).

Aidha, amesema wako wanaozalisha dawa hizo hivi sasa kwa kutumia hila hiyo, jambo ambalo lina athari kubwa kiafya kwa mhusika.

Kikwete alifichua hayo jana wakati alipokwenda kuwaaga wapanda mlima na waendesha baiskeli 61, walioanza safari ya siku saba ya kupanda Mlima Kilimanjaro.

Wapanda mlima hao wanashajihisha kampeni ya kitaifa ya kuchangia fedha za vita dhidi ya mapambano ya virusi vya Ukimwi (VVU) na Ukimwi.

"Dawa ni bure, ukisikia mtu anakwambia zinauzwa anakudanganya, hivyo chukueni kwenye vituo rasmi. Siku hizi watu wanafanya udanganyifu; wapo ambao wanaweka unga wa muhogo jambo ambalo lina athari kwa afya na haziwezi kumsaidia mhusika.

"Upo udanganyifu mwingi unaofanyika katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Ni wajibu wa watumiaji kuchukua dawa maeneo yanayoelekezwa na wataalamu wa afya hapa nchini," alisema.

Kuhusu vita dhidi ya Ukimwi, Kikwete alisema serikali imejipanga kununua mashine nyingi za kupimia kiwango cha virusi vya maradhi hayo katika mwili wa binadamu na kufafanua kuwa mashine hizo zinalenga kusaidia upatikanaji wa dawa kwa wakati na kuendelea kurefusha maisha. Kabla ya kuwaaga wapanda mlima hao, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS), Dk. Jerome Kamwela, aliwataka wanaopanda mlima na wanaoendesha baiskeli, kuhakikisha wanafuata maelekezo ya viongozi wao ili waweze kutimiza lengo.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML), Terry Strong, alisema kuna haja kwa kwa serikali ya Tanzania, kuongeza jitihada za kutunza nguvu kazi iliyopo kwa sasa.

Pia aliwataka wapanda mlima hao kuchukua tahadhari ili waweze kwenda na kurudi salama.

"Mwaka wa fedha uliopita, Ofisi ya Waziri Mkuu, kupitia TACAIDS, tulikuwa na bilioni 14 lakini kwa mwaka huu wa fedha, tumepata bilioni 25," alisema Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ummy Nderiananga.

Safari ya kupanda Mlima Kilimanjaro wenye urefu wa mita 5,895 kutoka usawa wa bahari, inawahusisha waendesha baiskeli 25 watakaotembea kilomita 240 kuuzunguka mlima huo, 36 wanaupanda mlima kupitia lango la Machame (whisky route).

**-Imeandikwa na Mary Mosha na Anjela Mhando**



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila (kushoto), akikabidhi kitita cha 200,000/- kwa mjasiriamali wa Soko la Kivukoni kama msaada uliotolewa na Taasisi ya Lalji Foundation kwa wajasiriamali wanawake 50, wenye thamani ya Sh. milioni 10, sokoni hapo, jijini humo juzi. Wengine ni Mkurugenzi wa Lalji Foundation, Imtiaz Lalji (wa pili kushoto) na Diwani Kata ya Kivukoni, Sharik Choughule. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri ataja manufaa bonde la Songwe kwa Tanzania, Malawi

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amesema kuna manufaa makubwa katika bonde la Mto Songwe kwa wananchi wa Tanzania na Malawi, hivyo amehimiza nguvu zaidi katika kuleta maendeleo yaliyojikita katika kuinua maisha ya wananchi wa nchi hizo.

Aweso ambaye ni Mwenyekiti Mwenza wa Baraza la Mawaziri wa Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe (SONGWECOM) , aliyasema hayo wakati akifungua mkutano wa pili wa baraza hilo uliofanyika jijini Dar es Salaam.

"Serikali ya Tanzania na Malawi, zinaweka nguvu kushirikiana katika kuendeleza bonde hili na tusipoteze nguvu ambazo zimeshatumika na kutufikisha hapa tulipo," alisema Waziri Aweso.

Alisema majadiliano rasmi kati ya serikali za Tanzania na Malawi kwa ajili ya ushirikiano katika bonde hilo na kutafuta ufumbuzi wa pamoja wa kudumu wa changamoto mbalimbali ikiwamo mafuriko yalianza tangu mwaka 1976.

Naye Waziri wa Maji wa Malawi, Abida Sidik, akizungumza katika mkutano huo, alisema bonde hilo litaendelezwa na kubadili maisha ya wananchi wa nchi yake imejipanga katika kufanikisha miradi itakayobuniwa na wataalamu kutoka pande mbili za nchi nufaika, Tanzania na Malawi.

Kijiografia, Mto Songwe ni sehemu ya Bonde la Ziwa Nyasa kwa upande wa Tanzania na mto huo unaanzia katika milima iliyoko wilayani Mbozi na kumwaga maji yake katika Ziwa Nyasa.

Aidha, Mto Songwe unaunda sehemu ya mpaka kati ya Tanzania na Malawi na una urefu wa kilometa 200. Bonde la Mto Songwe liko kusini magharibi mwa Tanzania na kaskazini mwa Malawi na lina ukubwa wa kilometa za mraba 4,243.

Pamoja na mapendekezo ya ujenzi wa mabwawa, usanifu wa kina umeandaliwa miradi 26 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 829 itakayotekelezwa kupitia Programu ya Kuendeleza Bonde la Mto Songwe.

Programu hiyo inashirikisha sekta mbalimbali zikiwamo maji, nishati, umwagiliaji, ardhi, kilimo, hali ya hewa, mazingira, serikali za mitaa, uwekezaji, viwanda na biashara.

# Mabula aipa kibarua NHC ujenzi wa nyumba

**Na Munir Shemweta**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amelitaka Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuangalia namna bora ya kutumia teknolojia ya kisasa katika ujenzi wa nyumba ili kujenga nyumba nyingi na kwa muda mfupi.

Dk. Mabula alisema hayo juzi wakati akikagua ujenzi wa mradi wa nyumba unaojulikana kama 'Samia Housing Scheme' unaotekelezwa na NHC kwenye eneo la Kawe, Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa Waziri Mabula, nchi zilizoendelea ziko kwenye hatua nzuri kwa kuwa ndani ya mwezi mmoja zinaweza kujenga nyumba 20 na NHC inatakiwa kupiga hatua kwa kuangalia mabadiliko hayo.

"Tunahitaji kujenga nyumba si tu kwa kutumia matofali tuliyo nayo bali kuwa na teknolojia nyingine itakayotuwezesha katika ujenzi wa nyumba nyingi na kwa muda mfupi lakini nyumba imara," alisema Dk. Mabula.

Hata hivyo, Dk. Mabula alisema mwaka ujao Tanzania itakuwa mwenyeji wa maonyesho ya kimataifa ya teknolojia ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu na kupitia maonyesho hayo, itajifunza kutoka kwa wengine.

Aidha, Waziri Mabula alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuiwezesha NHC kukopa fedha za kuendelea na miradi iliyosimama kwa muda mrefu.

Serikali iliruhusu NHC kukopa Sh. bilioni 173.9 na hadi sasa imekopa Sh. bilioni 44.7 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Kuhusu uhitaji wa nyumba nchini, Dk. Ma bula alisema kuwa, katika sensa iliyopita takwimu zinaonysha ni zaidi ya nyumba milioni 3.8 na kama ujenzi utafanyika kwa kasi basi zitahitajika kujengwa nyumba 500,000 kwa mwaka.

"Bado kuna uhitaji mkubwa wa nyumba na sehemu kubwa ya nyumba zinazojengwa na shirika letu la NHC watu wameonyesha nia ya kuzichukua na kwa mujibu wa sensa iliyopita upo uhitaji mkubwa wa nyumba katika jiji la Dar es Salaam," alisema.

Kwa mujibu wa Waziri, kupitia bajeti ya 2023/24 wananchi sasa wanaokwenda kununua nyumba za gharama nafuu wameondolewa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), hivyo nyumba ya Sh. milioni 50 kushuka chini itanunuliwa bila VAT.

Kutokana na hatua hiyo, Dk. Mabula aliweka bayana kuwa inachofanya serikali ni kuhakikisha nyumba za aina hiyo zinajengwa kwa wingi ili watanzania waweze kununua. Ametoa rai kwa watu wenye fursa ya kuendeleza ujenzi kufanya hivyo kwa kuwa uhitaji wa nyumba bado ni mkubwa.

NHC ilibuni mradi wa nyumba 5,000 za gharama nafuu wa Samia Housing Scheme zitakazojengwa kwa awamu katika mikoa mbalimbali nchini kwa gharama ya Sh. bilioni 466. Kwa kuanzia, shirika lilianzisha ujenzi wa nyumba 560 Kawe.


BIDCITY AUCTION & ESTATE SALES

House No. 44
Along Coca cola Rd
Mikocheni B
Opp. East Africa International School
Dar es Salaam - Tanzania

## NOTISI YA MNADA WA HADHARA

**BID CITY AUCTION & ESTATE SALES LIMITED,** Kwa idhini tuliyopewa na **KCB BANK TANZANIA LIMITED, MAKAO MAKUU, DAR ES SALAAM,** tutauza kwa Mnada wa hadhara dhamana za wadaiwa zilizo kwenye jedwali chini, endapo watashindwa kulipa madeni wanayodaiwa ndani ya muda wa siku ishirini na moja (21) kuanzia tarehe ya tangazo hili. Mnada utafanyika mahali zilipo dhamana hizo kama tarehe na muda ulivyoonyeshwa kwenye jedwali.

| | AINA YA DHAMANA | MAELEZO/SEHEMU ILIPO DHAMANA | TAREHE NA MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1 | HOTEL/ APPARTMENT | C.T No 97632, DAR, Kiwanja Namba 3, Kitalu Namba 25A, Mwanyamala, Kinondini, Ukubwa ni mita za mraba 489.04 | 05/08/2023, Saa 4:00 Asubuhi |
| 2 | NYUMBA | C.T No 41791, DAR, Kiwanja Namba 26, Kitalu "B" Kijitonyama, Kinondoni, Ukubwa ni mita 440 | 05/08/2023, Saa 6:30 Mchana |
| 3 | NYUMBA | C.T No 13583, MOSHI, Kiwanja namba 757, Kitalu "DDD" Ukubwa ni mita 540 | 05/08/2023, Saa 4:00 Asubuhi. |
| 4 | NYUMBA | Kiwanja namba 5/359, Reg 398, Mwembeladu Area, Nga`mbo District, Zanzibar | 06/08/2023, Saa 4:00 Asubuhi |
| 5 | NYUMBA | Kiwanja namba 26/511, Reg 293, Kwalaamsha Mjini, Zanzibar | 06/08/2023, Saa 6:00 Mchana |
| 6 | NYUMBA | C.T No 86330 DAR, Kiwanja Namba 952, Kawe, Kinondoni, Ukubwa ni Mita za mraba 1030. | 07/08/2023, Saa 4:00 Asubuhi |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei iliyofikiwa kwenye mnada endapo bei hiyo itakubaliwa na Benki na salio la 75% litalipwa ndani ya siku kumi na nne (14).
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio ndani ya siku 14, atakuwa amepoteza haki yake ya malipo ya 25% na dhamana itauzwa upya.
3. Gharama zote kuhusu kubadilisha jina na umiliki wa dhamana zitakuwa juu ya mnunuzi.
4. Baada ya kukamilisha maliyo yote ni jukumu la mnunuzi kumuhamisha mkazi/wakazi waliopo katika dhamana husika.
5. Dalali atawasilisha Benki bei iliyofikiwa katika mnada na Benki ina haki ya kukubali au kuikataa bei iliyofikiwa katika mnada.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi:**
**Bid City Auctions & Estates Sales Limited**
**House No.44 Mikocheni B, Coca Cola Road**
**Dar es Salaam**
**071381510/ 0719000002/ 0758182468**
**Adolf.mboya@bidcity.co.tz**

Phone: +255 712 759 377 +255 719 000 002
Mikocheni B | House No. 44 Along Cocacola Rd | Opp. East Africa International School Dar es Salaam - Tanzania
www.bidcity.or.tz info@bidcity.com

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kanuni Ligi Kuu 2023/2024 zisisahau maslahi ya Stars

**SHIRIKISHO** la Soka Tanzania (TFF) kupitia Bodi ya Ligi (TPLB), imetangaza msimu mpya wa Ligi Kuu Bara wa mwaka 2023/2024 utaanza rasmi ifikapo Agosti 15, mwaka huu kwa kushirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini.

Msimu huo mpya pia unatarajiwa kumalizika Mei 25, mwakani, kwa bingwa atakayeenda kupeperusha bendera ya nchi katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika kupatikana.

Timu zinazotarajiwa kuwania taji hilo ni pamoja na mabingwa Yanga, Simba, Azam FC, Singida Fountain Gate, Geita Gold FC, Tanzania Prisons, Dodoma Jiji, KMC FC, Coastal Union, Ihefu SC, Namungo FC, Kagera Sugar, Mtibwa Sugar, JKT Tanzania na Mashujaa FC.

Kabla ya bodi kutangaza kalenda ya msimu mpya, ilifungua dirisha la kupokea maoni kwa ajili ya kuboresha kanuni zitakazotumika katika msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi ya Championship, First League na Ligi Kuu ya Wanawake.

Kufunguliwa kwa dirisha hilo ni kunalenga kupokea maoni ya kuboresha pale palipoonekana pana mapungufu, lakini kuimarisha sehemu iliyoonekana iko vizuri katika msimu uliomalizika kuimarishwa zaidi.

Uamuzi huo unafanyika kwa ajili ya kujenga na kuzipa mafanikio zaidi ligi zote zinazoendeshwa chini ya usimamizi wa TFF na kuzifanya timu zinazopata nafasi ya kushiriki mashindano ya kimataifa kuwa katika kiwango bora. Ni wazi wachezaji wanaoshiriki katika ligi zinazoendeshwa katika usimamizi bora huwa na kiwango cha juu na pale wanapopata nafasi ya kucheza mashindano ya kimataifa wanakuwa tayari kupambana kwa sababu wamezoea mazingira hayo.

Tunaamini mbali na wadau wakiongozwa na viongozi wa klabu zinazoshiriki ligi hizo kuwasilisha maoni ambayo awali wanaamini yatawasaidia wao kwanza, lakini wanatakiwa kukumbuka na kuweka maslahi ya nchi mbele. Nipashe tunasema hili kwa sababu tunafahamu bado asilimia kubwa ya wachezaji wanaoitwa katika kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars), timu ya wanawake (Twiga Stars), na timu nyingine za vijana wanategemea wachezaji kutoka kwenye ligi hizo.

Kwa maana hiyo, wakati tunatoa maoni, tukumbuke pia uimara wa Taifa Stars, Twiga Stars na timu nyingine za taifa unapatikana kupitia ligi hizo, hivyo ni vyema zikawekwa kanuni zitakazosaidia kuimarisha vikosi vyetu.

Tukumbuke wakati tunaimarisha klabu zetu pendwa (Simba, Yanga, Azam, Coastal Union, Mtibwa Sugar n.k), ambazo kwa sasa zinapambana kupata matokeo chanya wanapokwenda kushiriki mashindano mbalimbali ya kimataifa, tusisahau U-Tanzania wetu ambao ndio kila kitu.


Kuna suala la idadi ya wachezaji wa kigeni wanaotakiwa kusajiliwa na timu za hapa nchini katika msimu mmoja, lakini kukiwa huru kwenye usajili wa mashindano ya kimataifa yanayosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), lakini likifanyika kutokana na uwezo wa klabu husika, tukumbuke bila Stars kufanya vizuri, hatusema tumepiga hatua kwenye mchezo huu wa kandanda. Hata hivyo ujio wa wachezaji wengi wa kigeni umesaidia kuipa hadhi Ligi Kuu Tanzania Bara hapa barani Afrika (sasa inashika nafasi ya tano), kwa sababu wamewapa ushindani wazawa kwa kuongeza juhudi ili kusaka namba katika vikosi vya timu wanazozitumikia.

Wachezaji wameamka na kufahamu wanatakiwa kupambana kuhakikisha wanaonyesha viwango vizuri ili kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara, lakini pia kujiongezea soko na thamani inapofika wakati wa kuboresha au kupewa mkataba mpya na timu ambayo inahitaji kupata huduma yake.

Tunazikumbusha klabu zote kutumia muda uliobakia kukamilisha mchakato wa usajili vizuri na kuwaandaa wachezaji kwa ajili ya kuanza msimu mpya, ni jambo lisilowekekana kwa timu ambayo haijafanya maandalizi sahihi ikavuna matokeo chanya. Timu zote ambazo zinatarajia kuchuana zinatakiwa kujipanga vyema katika kila idara kwa sababu mchezo wa soka hauhitaji miujiza, kusajili kikosi bora, kufanya maandalizi sahihi, kuboresha benchi la ufundi ni vitu muhimu vitakavyoisaidia klabu husika kufanya vyema katika msimu mpya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

### Klabu zijiimarishe, zijipange kuanzia mwanzo wa msimu

**ILE** hamasa na mwamko ulioonyeshwa na mashabiki wa Mashujaa FC katika mechi za 'play off' dhidi ya Mbeya City iliwashangaza na kuwafurahisha wadau wengi wa soka hata ambao hawakuwa mashabiki wa timu hiyo.

Pamoja na uwezo wa wachezaji uwanjani na mbinu za makocha, ukiangalia vyema mafanikio waliyopata, mashabiki wa Mashujaa FC wamechangia kwa kiasi kikubwa kufanikisha timu yao kupanda daraja na kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Hali hii ilionekana miaka 10 iliyopita wakati Mbeya City ilipopanda na kucheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza, ilikuwa na mashabiki waliokuwa wakiifuata na kuishangilia timu hiyo popote pale ilipokwenda, huku pia ikiwa na kikosi kilichokuwa kikifanya vizuri kwenye ligi.

Cha ajabu Mbeya City ilikuja kukumbushwa tabia ya mashabiki wao waliyokuwa nayo miaka 10 iliyopita na wenzao wa Mashujaa FC.

Ilianza kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma, umati wa watu uliofurika na kushangilia kwa staili ya aina yake mwanzo hadi mwisho wa mchezo na kuchangia kupata ushindi wa mabao 3-1.

Hali ile iliwashtua sana Mbeya City, na wao wakawa kama wamekumbushwa kitu, wakalipiza kwenye mechi ya marudiano.

Hata hivyo walichelewa kwa sababu mashabiki wa Mashujaa, wakafurika tena kwenye Uwanja wa Sokoine, Mbeya wakitokea Kigoma na aina ya ushangiliaji wao iliwazima kabisa wenyeji, wageni wakashinda bao 1-0.

Nimeandika haya nikiwakumbusha Mashujaa, hamasa hizi walizokuwa wanazifanya ziendelee tangu mwanzo wa ligi ili kuendelea kuisapoti timu yao.

Klabu nyingine nazo zinatakiwa ziige Mashujaa FC, kwani hivi sasa kumekuwa na tabia ya kutelekezwa hadi inapofikia kwenye hali mbaya ndipo wanasiasa, mashabiki na wadau wengine wanapojitokeza kwa kile wanachodai kuunda Kamati ya Ushindi ya kuinusuri timu kutoshuka daraja.

Mpaka tu kufikia hatua hii, tayari wanakuwa wameshachelewa na kinachofanyika ni kama kutaka ng'ombe anenepe siku ya mnada.

Niseme tu hii ni tabia timu nyingi kwenye Ligi Kuu hasa zile zinazoitwa au kujiita ndogo zikiongozwa na wakongwe, Coastal Union.

Ni wakati sasa wa kujirekebisha, kama ni hamasa au kujiweka vizuri kiuchumi, klabu zinatakiwa kujiandaa sasa na si kusubiri hali imekuwa mbaya kama ilivyokuwa kwa Mbeya City.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) kutoka Mbeya, Ndele Mwaselela, hivi karibuni alibainisha Mbeya City haikufanya vizuri msimu uliomalizika kutokana na kukosa motisha na hamasa ambavyo ni vitu muhimu kwenye soka.

"Kusema kweli timu yetu ilikosa motisha na hamasa na waliosababisha hivyo ni sisi wenyewe watu wa Mbeya, ikiwamo hata wanahabari, hawakuwa wanaeleza au kuandika na kuweka hadharani matatizo yanayoikumba klabu ili yatatuliwe, badala yake watu wakaona kila kitu kiko sawa tu, mnakuja kulaumu baada ya timu kushuka," alisema kiongozi huyo.

Nadhani timu nyingine ziige Mashujaa FC kwani pamoja na hamasa, imeanza kujiandaa kiuchumi na motisha baada ya Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, hivi karibuni kuwataka wabunge, wafanyabiashara na hata wasanii wanaotoka Kigoma kuichangia klabu yao ili ifanye vyema katika msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tuitie moyo timu yetu ili ikashindane, siyo kila siku kuziangalia Simba na Yanga kwenye TV, tunataka waje hapa, waje Lake Tanganyika, lakini tuanze jitihada za kuhakikisha uwanja wetu unakuwa mzuri, wananchi wa Kigoma nao wanastahili, wachezaji wanatoa wengi tu, vipaji vingi, kwa hiyo nawataka wabunge wawatafute wadau wote wa Kigoma, tuna wanamuziki mashuhuri kabisa katika taifa letu, wanaweza kuchangia siyo tu kuhamasisha tu timu zetu, lakini pia kukarabati ule uwanja wetu ufanane na Kigoma tunayotaka kuijenga," alisema Makamu wa Rais.

Hivi ndivyo inavyotakiwa na si kusubiri hali imekuwa mbaya ndiyo watu wanakusanyana kuisaidia timu isishuke, badala ya kuiwezesha kufanya vizuri tangu mwanzo wa ligi.

HABARI KITAIFA



Msimamizi wa Kitengo cha Ufundi wa Kampuni ya Mbolea ya Yara, Eddie Mija, akitoa maelezo kwa mawakala wa kampuni hiyo, kuhusu hatua za maandalizi ya mbolea, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadau wengi wavutiwa huduma za TBS

**Na Joseph Mwendapole**

TAASISI nyingi za serikali na binafsi zimevutiwa na huduma ya uthibitishaji wa mifumo iliyoanza kutolewa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Awali kabla ya Kitengo cha Usimamizi wa Ubora cha Shirika hilo kupata ithibati ya umahiri, huduma hiyo ilikuwa ikitolewa na taasisi za nje.

Ofisa Udhibiti Ubora Mkuu wa TBS, Mhandisi Yisambi Shiwa, alisema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu huduma zilizotolewa na shirika hilo kwenye Maonyesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, maarufu kama Sabasaba yaliyomalizika juzi kwenye Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam.

Mhandisi Shiwa alisema taasisi nyingi zimevutiwa na maelezo kuhusu kutolewa kwa huduma hiyo na shirika hilo baada ya kupata ithibati ya umahiri na zimeonyesha nia ya kuwasiliana na TBS ili kuthibitishia mifumo ya kimenejimenti.

Alitaja baadhi ya huduma za uthibitishaji wa mifumo zinazotolewa na TBS kuwa ni uthibitishaji wa Mfumo wa 'Quality Management System', uthibitishaji wa mifumo ambayo inasimikwa katika huduma za hoteli na nyinginezo ambazo zinajikita katika huduma za chakula. Mifumo mingine ni ile inayosimamia usalama wa mazingira na mifumo inayosimamia usalama na afya mahala pa kazi na zingine.

"Kwa sasa tunajivunia huduma hii ambapo TBS kupitia kitengo chake kinachohusika na usimamizi wa ubora imepata ithibati ya umahiri ya kuweza kudhibitisha mifumo mbalimbali na sasa taasisi nyingine zimeonesha nia ya kujapa kupata huduma hii," alisema Shiwa.

Kwa mujibu Shiwa, kabla ya TBS kupata ithibati ya umahiri ya uthibitishaji wa mifumo, huduma hiyo ilikuwa ikitolewa na taasisi za nje ya nchi, hivyo ilikuwa ni gharama na kulikuwa na changamoto hasa wakati wa majanga kama kipindi cha UVIKO-19 kwa kuwa ilikuwa vigumu watu wa taasisi hizo kusafiri kuja nchini kutoa huduma.

"Kwa hiyo taasisi za hapa nchini zilikosa hizo huduma walizokuwa wanapata kutoka nje kutokana na wafanyakazi wa taasisi hizo kushindwa kusafiri kuja nchini," alisema.

Alisema kwa sasa wana uhakika wa kupata huduma hizo kwa gharama nafuu na ina wataalamu waliobobea katika sekta hiyo na serikali inaendelea kuimarisha idara hiyo.

Naye Ofisa Udhibiti Ubora Mwandamizi wa TBS, Hassan Juma, alisema tangu maonesho hayo yameanza wamepokea wajasiriamali pamoja na wafanyabiashara wakubwa kwa mwitikio mkubwa na walielimishwa kuhusiana na huduma zinazotolewa na shirika.

Alitaja miongoni mwa huduma hizo kuwa ni uandaaji viwango, uthibitishaji ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini na nje ya nchi.

Aidha, alitaja huduma nyingine kuwa ni ya usajili majengo yanayojishughulisha na uuzaji wa vyakula na vipozi, huduma ya ukaguzi wa bidhaa zinazotoka nje ya nchi na kuthibitisha mifumo mbalimbali.

## BoT yajipanga kutekeleza mpango wa tatu wa taifa

**Na Pilly Kigome**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imesema iko katika mikakati ya kutekeleza Mpango wa Tatu wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Kifedha unaotekelezwa kwa miaka sita kuanzia mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari hivi karibuni, Ofisa wa BoT, Huduma za Kurugenzi ya Ujumuishi na Ustawi wa Huduma za Fedha, Lucas Maganzi, alisema benki hiyo pia, inatoa fursa ya kushirikisha wabunifu na kampuni katika teknolojia ya masuala ya kifedha, ili kupata ubunifu ambazo zitatumika katika masuala ya kifedha.

Alisema wametoa fursa hiyo ili watu na kampuni zijitokeze kutoa ubunifu wao ambazo zitakusanywa na zitakazofaa zitapendekezwa na kutumika kisheria.

Maganzi alisema kurugenzi hiyo ina majukumu makubwa matano likiwamo la kuratibu utekelezaji wa mpango na kutekeleza mikakati ya wadau kutoka sekta binafsi na umma ambapo mwenyekiti wake ni Gavana.

Alisema wamekuwa wakitekeleza mpango huo ulioanza mwaka 2018 na kumalizika mwaka 2022.

Pia alisema wanahakikisha wanachochea ubunifu za teknolojia mbalimbali katika huduma za kifedha na BoT ipo katika hatua ya kuanzisha mazingira ya majaribio kuruhusu watu na kampuni kuzipeleka na zitakazokubalika zitumike kisheria.

Aidha, alisema Kurugenzi hiyo inaratibu utoaji wa elimu ya fedha kwa umma ikihusisha za akiba, mikopo na uwekezaji kupitia idara ya mawasilino BoT.

Kadhalika, alisema wanahakikisha wananchi wanafikiwa na kutumia huduma rasmi za kifedha ambazo zinatambulika kisheria na zinazosimamiwa na wadhibiti wa fedha.

# Watoto 14,000 huzaliwa na tatizo la selimundu kila mwaka

**Na Gwamaka Alipipi**

KILA mwaka watoto 14,000 nchini huzaliwa wakiwa na matatizo kwenye chembe chembe nyekundu za damu zao na hivyo kupata ugonjwa wa selimundu (sickle cell).

Hali hiyo inaifanya Tanzania kuwa nchi ya tano duniani kwa kuwa na idadi kubwa ya wagonjwa wa selimundu, huku nafasi ya kwanza ikishikwa na Nigeria, India (pili), Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) (tatu) na Uganda (nne).

Hayo yalibainishwa juzi jijini Dar es Salaam na Mganga Mkuu wa Serikali, Profesa Tumaini Nagu, wakati wa ufunguzi wa kongamano la selimundu, uzinduzi wa chapisho maalum la magonjwa ya damu na selimundu.

Profesa Nagu alisema selimundu ni ugonjwa wa kurithi na kwa Tanzania umekuwa ni tatizo kubwa kutokana na kuenea kwa kasi.

Alisema asilimia saba ya vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano nchini vinachangiwa na ugonjwa huo.

Alisema kutokana na hali hiyo, serikali imeanza kufanya jitihada mbalimbali za kupambana na ugonjwa huo mojawapo ni kuutambua ukiwa katika hatua za awali.

"Kwa sasa hivi hospitali zote saba za kanda nchini zimeanza kutoa huduma za utambuzi na tiba, hadi mwaka 2015 Hospitali ya Taifa Muhimbili ilikuwa ndiyo pekee inayokuwa ikitoa huduma hiyo," alisema Profesa Nagu.

Alisema serikali pia imeanza mkakati wa kuhakikisha matibabu ya watoto wenye ugonjwa wa selimundu yanakuwa bora na mazuri.

Profesa Nagu alisema hatua nyingine ni kuhakikisha kunakuwapo na dawa katika hospitali zote ikiwamo katika Bohari ya Dawa (MSD), dawa aina ya hydroxyurea wanayopewa waathirika wa ugonjwa huo inatengenezwa hapa nchini.

"Hii dawa ya hydroxyurea ndiyo wanayopewa wagonjwa wa selimundu, sasa mkakati wa serikali ni kuhakikisha dawa hii inakuwapo katika mwongozo wa dawa na inapatikana kwa urahisi," alisema Profesa Nagu.

Alisema mkakati mwingine ni kuwapo na matibabu ya upandikizaji wa uroto.

"Mei mwaka huu Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alizindua huduma ya upandikizaji uroto katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, sasa itaanza kupatikana Hospitali ya Taifa Muhimbili. Serikali katika bajeti ya mwaka 2023/24 imetenga zaidi ya Sh. bilioni tano kwa ajili ya kusaidia upandikizaji uroto."

Kadhalika alisema mkakati mwingine ni wagonjwa wa selimundu kupewa damu.

Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Profesa Appolinary Kamuhabwa, alisema wamekuwa wakifanya utafiti wa magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza, lengo kuu ni kusaidia serikali katika kudhibiti na kutibu.

"Utafiti wetu umejikita katika kuzuia, kuchunguza, kutibu, upandikizaji wa uroto ni sehemu ya utafiti wetu."

Kwa mujibu wa Prof. Nagu, MUHAS kazi yao ni kuandaa wataalamu wa afya ambao watakwenda kutibu magonjwa mbalimbali ikiwamo selimundu.

# Harakati za kisiasa, upotoshaji sumu kwa uwekezaji wa bandari

Na Mwandishi Wetu

JUNI 13, mwaka huu, Katibu Mkuu wa zamani wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na Balozi wa zamani wa Tanzania nchini Sweden, Dk. Willibroad Slaa, alifanya mkutano na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam.

Mkutano huo ulifanyika wakati vuguvugu la suala la uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam na kilicholengwa na mwanasiasa huyo ni kupinga mpango huo wa serikali. Dk. Slaa na watu wengine wanapinga suala hilo kwa kile wanachodai kuwa ni kuingiliwa kwa raslimali za nchi.

Pamoja na kupinga huko, kundi hilo la watu linashindwa kuweka bayana ni manufaa gani yanayoweza kupatikana kutokana na mpango huo wa serikali. Kwa maneno mengine wanasukuma agenda ya kukwamisha wazo la uwekezaji wa DP World.

Ili kutoa huduma nzuri licha ya changamoto kubwa zilizoikumba bandari yetu, suala la uendeshaji wa rasilimali hiyo, lilitoa mwanya kwa baadhi ya watu kuneemeka kwa kuendesha baadhi ya vitengo bandarini na kuwapatia fedha nyingi. Kwa maana hiyo, suala la uendeshaji wa bandari kwa kushirikiana na wabia si geni bali lilianza zamani.

Mfano ni kampuni ya Tanzania International Container Terminal Services (TICTS) ambayo ilipewa kazi ya kuendesha kitengo cha makontena. TICTS ilikodishwa kuendesha gati namba Nane hadi 11 na imemaliza mkataba uliodumu kwa miaka 22. Watu kama hao hawawezi kuridhia kuachia fursa hiyo kirahisi hata kama haonekani wakipinga hadharani lakini itoshe kusema wanaumia.

Wako wengine waliokuwa wanatoa huduma ya vituo vya makasha vya nchi kavu (ICD) na wengineo. Hawa nao hawawezi kukaa pembeni kirahisi.

Kama hiyo haitoshi, taifa haliwezi kupendwa na kila nchi tunayopakana nayo. Hivyo kuiboresha Bandari ya Dar es Salaam, ni sawa na kuangamiza bandari za majirani hasa Kenya. Nani asiyejua ushindani wa kiuchumi kati ya Tanzania na Kenya?

Wapinzani wa kibiashara hawashindwi kuchomeka hoja binafsi kwa kutumia watu wa ndani kwa lengo la kupunguza nguvu za kiutendaji kwenye rasilimali za nchi kutooana na kuhofu kwamba wanaweza kuzidiwa kete kibiashara na Tanzania kunufaika kiuchumi.

Haya yanafanyika wakati Rais Dk. Samia Suluhu Hassan anaendesha mambo kwa uwazi, busara na ushirikiano wa kila mmoja. Rais Samia anafanya siasa za kutibu majeraha kwa nia ya kuwaunganisha wote.



Dk. Willibroad Slaa

Wakati hayo yakifanyika, ni dhahiri kwamba kuna watu wasiopenda Tanzania ikipiga hatua kimaendeleo, hivyo wanafanya kila njia kuhakikisha azma hiyo inatimia.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba hivi karibuni Bunge lilipitisha bajeti ya Sh. trilioni 44.39 kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo kwa mwaka 2023/24, Bajeti hii itatoka kwenye vyanzo vya ndani na nje.

Vyanzo vya ndani ni pamoja na makusanyo yanayotokana na mapato ya bandari ambayo kwa sasa yanakadiriwa kuwa Sh. trilioni saba. Kama hiyo haitoshi, wataalamu wa uchumi wanasema muundo utakaowekwa katika bandari, chini ya DP World, mapato ya bandari yanakadiriwa kuwa Sh. trilioni 26 ambazo ni mara tatu zaidi ya fedha zinazopatikana kwa sasa.

Kwa mantiki hiyo, uwekezaji huu utainufaisha nchi kwa kiasi kikubwa.

Endapo serikali itachukua maoni mazuri ya wananchi wenye nia nzuri na taifa, si haba nchi itapiga hatua. Iwapo hili halitatazamwa kwa kina, nchi itafanya makosa makubwa kuruhusu siasa zipenyezwe kwa jambo kubwa la kiuchumi.

Tukirudi kwenye msingi wenyewe wa mwelekeo wa uwekezaji wa bandari kupitia DP World, malalamiko, hujuma na dhihaka kwa wakosoaji zinakosa (legitimacy) yaani uhalali wa kulishambulia wazo lenyewe kwa sababu zinachochewa na kisiasa.

Hapa lazima tuelewe mambo kadhaa ambayo Watanzania wanapaswa kuelezwa kwa mapana. Mpaka sasa, hakuna mkataba uliowekwa wa uwekezaji wala hayo mauziano kama inavyopotoshwa.

Kilichofanyika mpaka sasa ni mjadala wa ushirikiano kati ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) na Kampuni ya DP World kutoka Umoja wa Falme za Kiarabu kupitia mkataba mdogo wa Inter-governmental Agreement (IGA) baina ya Tanzania na Dubai. Kwa picha halisi ni kuwa baadaye kutakuwa na mkataba rasmi baada ya pande zote mbili kukubaliana na kuainisha maeneo husika ya kiuwekezaji.

Jambo wanalotakiwa Watanzania kuelewa ni kwamba Juni 10, mwaka huu, wabunge hawakujadili mauziano, bali mpango wa uwekezaji unaoungwa mkono na Katiba ya Tanzania Ibara ya 63, ibara ndogo ya 3 (e) inayoelekeza mikataba ya kimataifa kuridhiwa bungeni.

Bahati mbaya sio mikataba yote iliyowahi kupelekwa bungeni kama huu wa DP World. Hii inatokana na aina ya uongozi wa Rais Samia kuweka wazi mikataba kwa Taifa letu. Hata mikopo ya Kimataifa inayorefusha deni la Taifa, anaiweka wazi. Hafichi kama ilivyokuwa kwa mtangulizi wake hayati Dk. Magufuli.

Spika wa Bunge wa Tanzania, Dk. Tulia Ackson, aliwatoa hofu Watanzania kuhusiana na ujio wa DP World.

"Makubaliano haya yanaruhusu mabadiliko ama marekebisho (Fungu la 22 ama ibara ya 22). Makubaliano haya yanaweza kusitishwa asikuambie mtu tumeingia miguu yote miwili, kifungu cha 23 kinaruhusu upande wowote kusitisha," alisema Spika Dk. Tulia.

Hivyo ukweli halisi unajulikana. Wanaozua hofu kwa Watanzania, wana malengo yao. Kamwe sio uzalendo kama wanavyojaribu kuwaaminisha Watanzania.

Wananchi wapaswa kujua bandari haijauzwa kama inavyoenezwa.

Makubaliano ya awali yanatoa muda miezi 12 ya maridhiano. Pindi muda huo utakapokwisha na kusipokuwa na mwendelezo, hakutakuwa na uwezekano wa DP World kupewa mkataba huo.

Ushahidi huu upo kwenye kipengele cha 23 (3) cha makubaliano ya awali yanayopigiwa kelele na wachonganishi wa Taifa. Kipengele hiki kinagusia taratibu za uvunjwaji wa mkataba huo.

Wanachokifanya wanaopinga mkataba huo, yaani wanasiasa na baadhi ya wanasheria ni agenda za siasa ambazo hazina mashiko katika vita hii kubwa na ngumu ya kiuchumi.

Kitakachofanyika ni maboresho ya bandari, si mauziano. Watanzania wengi wanahitaji kuona meli zinakaa kwa saa chache wakati wa upakuaji wa mizigo na si wiki moja au mbili na kuongeza gharama kwa watumiaji wa bandari. Mbaya zaidi gharama hizi zinahamia kwa watumiaji wa bidhaa zinazoingizwa na meli hizo kwa kupaisha bei ya bidhaa maradufu.

Ni bandari hii ambayo tulishuhudia kampuni kutoka Hong Kong ikifanya shughuli zake hapa nchini kama TICTS kwa miaka 22. Kama TICTS hawakuuziwa, DP World wanauziwaje? Ni ajabu wanaopinga wanashindwa kuona faida ya uwekezaji bora wa bandari.

Mpaka sasa gharama ya meli kusubiri kuingia nangani ni Dola 25,000 sawa na Sh. milioni 58 kwa siku. Kama hiyo haitoshi, meli moja inachukua hadi siku tano kushusha mzigo badala ya siku moja inayotakiwa kimataifa. Kwa hiyo ujio wa wawekezaji mfano wa DP World katika Taifa letu ni jambo la kujivunia kwa mustakabali wa nchi yetu.

Kuboreshwa kwa bandari hii kutapunguza gharama za utumiaji na kuongeza pia idadi ya meli zitakazokuja bandari ya Dar es Salaam kutoka meli 1,569 zilizohudumiwa mwaka 2021/22 hadi kufikia takriban meli 2,950 ifikapo mwaka 2032/33.



## Wizara yaweka mikakati kusaidia wenye ulemavu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum imejizatiti katika kuhakikisha inasaidia wanawake hasa wenye ulemavu kupata fursa mbalimbali za kujikwamua kiuchumi kwa kupata mikopo kwa ajili ya mitaji ya shughuli za kiuchumi.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Amon Mpanju, alisema hayo jana alipokutana na kuzungumza na uongozi wa Shirikisho la Vyama vya Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) jijini hapa.

"Tuna Idara ya Maendeleo ya Jinsia hapa wizarani. Mkurugenzi husika hakikisha mnaandaa mkutano wa wanawake wenye ulemavu nchini kujua changamoto zinazowakabili katika masuala ya mikopo na uwezeshaji wa kiuchumi," alisema Mpanju.

Alipongeza Shirikisho la Benki Tanzania kwa kuboresha miundombinu ya benki na baadhi ya mifumo ambayo imekuwa msaada kwa watu wenye walemavu.

Naye Katibu Mkuu wa SHIVYAWATA, Jonas Lubago, aliiomba serikali kuboresha utoaji wa mikopo hasa ile ya asilimia 10 ambayo asilimia mbili ni kwa watu wenye ulemavu inayotolewa na mamlaka za serikali za mitaa.

Luboga aliishukuru wizara hiyo kwa ushirikiano inaowapatia kupitia wataalamu mbalimbali katika kuhakikisha watu wenye ulemavu wanashiriki shughuli za kijamii na hasa za kuwasaidia kujikwamua kiuchumi.

# Uanzishaji ranchi kuleta mageuzi mifugo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema serikali imedhamiria kufanya mageuzi makubwa kwenye sekta ya mifugo ikiwamo kuwa na ranchi ndogo na kutoa fursa za ajira kwa vijana na wanawake.

Aidha, amesema tangu Rais Samia Suluhu Hassan kuifungua nchi kiuwekezaji, kumechochea ongezeko la biashara ya nyama nje ya nchi na kwamba tani 12,000 za nyama zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 51, zimeuzwa ikilinganishwa na mwaka 2020 ziliuzwa tani 1,600.

Ulega aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ushirikiano wa wizara hiyo na Chuo cha Kimataifa cha Utafiti wa Mifugo(ILRI) na maandalizi ya kuelekea Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF 2023) litakalofanyika Septemba 5 hadi 8, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Waziri Ulega alisema mkakati uliopo ni kuwa na ranchi za asili 1,000 ili kuchochea ufugaji wenye tija na zitasajiliwa ili kurahisisha uuzaji wa nyama nje ya nchi.

Alisema katika mazungumzo yake na Mkurugenzi wa ILRI, amempa mambo sita ya kushughulikia ikiwamo kutafakari kwa pamoja namna ya kuwawezesha vijana na wanawake kushiriki kikamilifu katika sekta ya mifugo na uvuvi.

Alisema wamekuwa na mazungumzo ili kuchagiza sekta ya mifugo ambayo pamoja na kuwa na mifugo mingi lakini bado haifanyi vizuri.

"Tunataka sekta ya mifugo ichangie fedha nyingi za kigeni lakini ni fursa nzuri kwa vijana wetu kushiriki kwenye sekta hii. Hii inatokana na maono ya Rais Samia Suluhu Hassan anayetaka kuona tunafanya kazi ya kuwashirikisha vijana na kinamama kwenye hili eneo," alisema.

Alibainisha kuwa tayari serikali imejipanga kuwa na vituo kwa ajili ya vijana kwenye sekta ya mifugo, uvuvi na ujasiriamali kwenye mikoa ya Mwanza, Kagera na Tanga. "Kwenye hivyo vituo vya BBT lazima kuzungumzia kiteknolojia, kijana anataka kuuza ngombe wake kuwe na APP auze ngombe wake duniani, kama ni ugonjwa unasumbua kijana apate huduma ya mifugo yake kiganjani, kufungua masoko zaidi nje, hawa ILRI wana majibu ya kitaalamu waliyofanyia utafiti kwa muda mrefu," alisema.

Alisema chuo hicho kina uzoefu mwingi, utafiti mwingi uliofanyika utakaosaidia sekta hiyo kupiga hatua kwa kuwa inahusisha Watanzania wengi.

"Kwa hiyo tumekubaliana haya yote tufanye pamoja na pia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, nashukuru hii ILRI Tanzania kwa kuendelea kushirikiana tumejipanga mifugo lazima iingize fedha za kigeni nchini.

"Tunataka kufanya mageuzi makubwa tuondoke kwenye uchungaji wa kiasili na kwenda kumiliki ranchi ndogo ndogo zitakazochochea mageuzi hayo," alisema.

Kuhusu malisho, alisema kuna zaidi ya mashamba 100 kwenye halmashauri 42 na kusisitiza eneo hilo linahitaji wawekezaji hivyo kupitia jukwaa hilo alitoa wito kwa wawekezaji kuwekeza.

"Eneo la biashara ya majani tunataka kulipigia kelele sana watu waamini eneo hili nalo ni fursa, lakini pia tunatoa elimu kwa wafugaji kuvuna mifugo ili kuondokana na ufugaji wa asili na changamoto ya malisho," alisema. Akizungumzia jukwaa la AGRF 2023, Waziri Ulega aliishukuru Taasisi ya Kuendeleza Kilimo Afrika (AGRA) ambao ni waandaaji wa kuu wa jukwaa hilo ambalo usajili wa wadau watakaoshiriki unaendelea kwa sasa na mwisho ni Agosti mosi mwaka huu.

"Mkutano huu Watanzania watakapa fursa ya mitaji na masoko, kuna fursa nyingi za wageni watakaokuja nchini, Tanzania ipo tayari kupokea mkutano huu na Tanzania ipo tayari kwa uwekezaji.

"Tunataka kuona vijana na kinamama wananufaika kwa kuzalisha maziwa, biashara ya kuku, tunataka kufanya miradi mikubwa iende hadi kwa akina mama kule vijijini sio kuishi na kuku bali kufanya biashara ya kuku," alisema.




Mkuu wa Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, Gift Msuya, akifungua mkutano wa wadau wa kujadili mpango wa matumizi ya ardhi ulioandaliwa na mradi wa uboreshaji usalama wa milki za ardhi wilayani humo jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Jumuiya CCM yataka mila, desturi katika malezi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

JUMUIYA ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Singida imewataka wazazi kuwalea watoto wao kwa kufuata mila na desturi za Kitanzania ili kudhibiti tatizo la mmomonyoko wa maadili kwa vijana.

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Bertha Nakomolwa, aliyasema hayo juzi wilayani hapa kwenye ziara ya chama hicho ya kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali kupitia ilani ya chama hicho.

Alisema hivi sasa utandawazi na mitandao ya kijamii imekuwa chanzo cha vijana kuwa na maadili mabaya hivyo wazazi wawe karibu na watoto wao.

Naye Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Singida, Martha Mlata, alisema serikali inaendelea kutatua kero zinazowakabili wananchi kwa kutekeleza miradi mbalimbali kwenye maeneo yao kwa lengo la kusogeza huduma karibu nao. Mlata aliwataka wananchi kuitunza miradi inayotekelezwa katika maeneo yao ili idumu kwa muda mrefu na vizazi vijavyo viweze kuitumia kwa kupata huduma. Baadhi ya wananchi wa Kata ya Ughandi walisema wanakabiliwa na kero ya barabara ambayo inatoka Ughandi hadi Msisi kwa haipitiki hasa kipindi cha masika.

Mbunge wa Singida Vijijini, Ramadhani Ighondo, alisema ubovu wa barabara hiyo imekuwa tatizo kubwa sana hali inayosababisha kina wajawazito kujifungulia njiani.





# Hemed afurahishwa kasi ujenzi masoko

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, amekagua maendeleo ya ujenzi wa miradi ya masoko ya Mwanakwerekwe, Jumbi na Chuini, Mjini Magharibi na kufurahishwa kuona wasimamizi na mkandarasi ni wazawa wenye uzalendo.

Akizungumza katika ziara hiyo jana, alisema ujenzi wa masoko hayo ni mwendelezo wa kuwawekea ustawi wananchi kwa kuwasogezea huduma bora karibu na maeneo wanayoishi.

Hemed alisema kukamilika kwa ujenzi wa miradi hiyo kutatatua changamoto ya wananchi kufuata huduma mbali na makazi yao na wafanyabiashara kufanya shughuli zao katika masoko ya kisasa yenye ubora na viwango.

Makamu wa Pili wa Rais alivipongeza vikosi vya ulinzi na usalama ambavyo vimepewa dhamana ya kujenga masoko hayo pamoja na Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA) kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Massoud Ali Mohammed, alisema baada ya kukamilika, katika soko la Mwanakwerekwe zaidi ya wafanyabiashara 4,000 watanufaika na katika masoko ya Jumbi na Chuini, zaidi ya wafanyabiashara 4,500 watanufaika.

Mshauri Mwelekezi na Msanifu Majengo kutoka ZBA, Shadya Fauz Mohd, alisema wataendelea kusimamia na kujenga miradi yote kwa ubora na viwango vinavyokubalika ili kuyawezesha masoko hayo kutumika kwa muda mrefu.

# Zanzibar kutangaza utalii kivingine

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIKA kuitangaza Zanzibar kwa maendeleo ya utalii wa michezo, imeandaa mashindano ya mbio za riadha (Zanzibar International Marothon) yatakayofanyika Oktoba, mwaka huu, ili kushajihisha maendeleo ya michezo kwa vijana, wanawake na watoto.

Uzinduzi wa mashindnao hayo ulifanyika juzi visiwani hapa na Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita.

Katika uzinduzi huo, Waziri alisema serikali itaendelea kuhakikisha mashindnao hayo yanakuwa ya aina yake ili kuitangaza Zanzibar katika sekta ya utalii.

Waziri Tabia alisema mashindnao hayo yatasaidia kuitangaza Zanzibar duniani na kupongeza ubunifu huo ambao utakuza utalii wa kimichezo.

"Katika kuendeleza sera ya michezo ya mwaka 2017/18 imetutaka kusimamia michezo kwa wote wakiwamo watu wenye ulemavu, hivyo wizara tutahakikisha tunasimamia pasipo kujali jinsia, dini wala rangi. Watu wote washiriki katika michezo," alisema.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Meneja Mauzo wa Kampuni ya Simu ya TIGO/Zantel Zanzibar ambao ndio wadhamini wakuu wa mashindano hayo, Muhammed Wakil, alisema anaamini mbio hizo zinatoa jukwaa bora kutangaza utalii, kukuza vipaji vya wanariadha, kuimarisha afya na kuchangia uchumi wa buluu.

Alisema dhamira yao ni kuendelea kuleta mabadiliko chanya kwenye jamii kwa kuwekeza kwenye miradi inayogusa hisia za wananchi na hawawezi kufanikiwa bila kushirikiana na wadau wengine na serikali katika kuwafikia wanajamii katika uwekezaji.

Kampuni hiyo, alisema licha ya kuwekeza katika jamii, inaendelea kuwekeza katika miundombinu za mawasiliano ili kutoa huduma bora za mawasiliano kwa wateja wao na ndio wa kwanza kuleta teknolojia ya 4G na 5G yenye kazi kubwa na kuanzisha simu janja kwa mkopo nafuu ili wananchi kumiliki simu.

Pia alisema kwa kushirikiana na serikali pia kampuni hiyo imejenga minara 45 mipya ya mawasiliano Unguja na Pemba na kuungana na vyama vya wakulima wa karafuu Pemba kwa ajili ya kurahisisha malipo yao kupitia Tigo Pesa.

"Tunampongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa kuweka mazingira rafiki kwa wadau mbalimbali kuwekeza Zanzibar," alisema meneja huyo. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, alisema Wazanzibari wanapaswa kuyaunga mkono yale ambayo yanatokea kwao yakiwamo mashindano hayo ya riadha badala ya kuwabeza wale wanaoandaa ili kufaidika na fursa zilizopo.

Alisema ubunifu huo utasaidia kukuza uchumi hasa ikizingatiwa kuwa Zanzibar ina uchumi wa huduma ya utalii, hivyo uchumi huo unahitaji matukio na utalii kuwa endelevu.

Naye Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Hussein Ghulam, alisema katika mbio hizo wizara itatoa mchango kwa kuhakikisha vyuo mbalimbali vinashiriki pamoja na wanafunzi wa sekondari.

"Imani yangu kufanya hivyo kile ambacho kitapatikana maana yake Zanzibar Marathon itaunga juhudi za viongozi katika kuboresha miundombinu katika sekta ya elimu," alisema.




Katibu wa Tume ya kurekebisha sheria Zanzibar, Mussa Kombo, akizungumza na waandishi wa habari, mjini Zanzibar jana, kuhusu mchakato wa serikali ya mapinduzi wa kuwa na sheria ya taarifa za mtu binafsi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Zanzibar yakiri haina sheria ya kulinda taarifa binafsi za watu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ZANZIBAR imesema haina sheria inayotoa ulinzi wa taarifa binafsi za watu licha ya kuwapo kwa sheria nyingi zinazotaka kutoa taarifa na kuwasilisha katika mamlaka tofauti.

Akizungumza jana visiwani hapa katika kikao cha utoaji wa elimu kwa waandishi wa habari na asasi za kiraia kuhusu sheria ya ulinzi wa taarifa binafsi za watu, Katibu wa Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar, Mussa Kombo, alisema nchi mbalimbali zinatoa ulinzi wa taarifa binafsi za watu, hivyo ni vyema na Zanzibar kuwa na sheria hiyo.

Alisema wananchi wanatoa taarifa zao binafsi bila kuwa na ulinzi utakaowalinda kisheria na kutolea mfano wa wale wanatoa taarifa zao kwa kina kwa wataalamu wa afya hasa wanapofuata huduma za afya.

"Kwa mfano leo ukipeleka taarifa zako binafsi hospitalini unamweleza daktari kila kitu chako ili kupata tiba sahihi na wakati mwingine utaeleza mpaka mambo ya siri. Inawezekana mwenza wako usimwambie lakini daktari unamweleza ili kupata tiba sahihi lakini kwa bahati mbaya hatuna ulinzi wa taarifa hizo," alisema.

Tanzania Bara, alisema imeshapitisha sheria ya kulinda taarifa binafsi kwa wananchi na ikitokea taarifa zao zimevuja kuna haki ya kupata fidia.

Alisema wananchi wa Zanzibar wanatoa taarifa zao binafsi katika mamlaka mbalimbali lakini hakuna utaratibu mzuri wa kisheria wa kuzilinda taarifa hizo zisitoke mahali pengine kinyume cha zilivyokusudiwa.

"Zanzibar hatuna sheria zinazosimamia masuala ya ulinzi wa taarifa zetu binafsi. Ukienda Uingereza wanayo sheria hii tokea mwaka 1999. Tanzania Bara wanayo, Kenya tayari, Uganda tayari na nchi nyingi wanayo, hivyo hawa wote wanaokusanya taarifa zetu hakuna sheria inayotulinda," alisema.

Pia alisema wananchi wanawasilisha taarifa zao kwa baadhi ya mamlaka wakiamini zitahifadhiwa vizuri lakini inatokea taarifa hizo zinatoka kwa sababu ya kutokuwa na utaratibu mzuri.

Hata hivyo, alisema tume hiyo imepitia sheria mbalimbali zinazotoa mamlaka ya kukusanya taarifa za wananchi ikiwamo sheria ya usajili wa matukio ya kijamii, sheria ya hospitali, sheria ya mikopo ya elimu ya juu ili kujua ulinzi wa taarifa hizo na kubaini kuwa hakuna ulinzi wa moja kwa moja.

"Pia tumebaini kuwa hakuna utaratibu wa kuwafidia watu ambao taarifa zao zimevuja iwe kwa bahati mbaya au makusudi," alisema.

Kadhalika, alisema wameangalia uzoefu wa nchi mbalimbali ndani na nje ya Afrika Mashariki kuona walindaje haki ya taarifa binafsi na nchi nyingi zimeweka ulinzi wa taarifa hizo lakini Zanzibar iko nyuma kwa kukosa sheria hiyo.


Katibu huyo alisema wawekezaji wanapowekeza katika nchi mbalimbali, moja ya mambo wanayoyatizama ni pamoja na mfumo wa sheria husika na kutolea mfano wanaweza kutazama faida watakazozipata watakapowekeza lakini wakabaini Zanzibar inakosa sheria ya taarifa ya ulinzi binafsi, inaweza kupata athari kwa kutokuwa na sheria hiyo.

Alisema tume imekuja na mapendekezo kuishauri serikali kutunga sheria hiyo ili kuwa na ulinzi wa kutosha wa kulinda taarifa za wananchi na kuwa na kuwahakikishia wawekezaji taarifa zao zitadhibitiwa na kuhifadhiwa kisheria.

Alisema sheria hiyo ikapopitishwa itasimamia usawa wa kutowaonea watu na kupata ulinzi wa taarifa zao lakini pia taasisi itakayotoa taarifa italazimika kumlipa fidia mlengwa taarifa zake zilizovujishwa.

Naye Mratibu wa Taasisi ya Cente for Youth Dialogue, Ali Shaban Mtwana, alisema serikali inatoa ushirikiano kwa asasi za kiraia katika kuhakiksiha zinatoa mchango kwa ajili ya marekebisho na kuleta ushawishi wa sheria mpya ambazo zitasaidia jamii.

Alisema msingi wa ushirikiano huo kuweka mazingira mazuri hasa kwa wananchi kupitia kazi na majukumu yao kupitia taasisi ya kurekebisha sheria.



**DIAMOND**
UKURASA 12

Nipashe MWANGA WA JAMII
BT BURUDANI TELE
JUMAMOSI JULAI 15, 2023



# PENGINE INAKUJA

MALKIA wa Bongo Muvi, Wema Sepetu, hatimaye ameyatoa ya moyoni baada ya kuwapo kwa taarifa kuwa hivi karibuni anatarajia kupata mtoto.

Kupitia kwenye ukurasa wake wa Instagram, mrembo huyo ambaye kwa sasa anaishi na msanii wa muziki Whozu, ameamua kujibu ukweli wake baada ya watu kuanza kumtumia jumbe za kumpongeza.

Chanzo cha yote kilianzia baada ya picha yake kusambaa akionekana akiwa na tumbo kubwa na kuashiria ni mjamzito na anatarajia kujifungua miezi michache inayokuja.

Watu walimpongeza na wengine kumtakia kila mema ili ajifungue salama ajifute machozi kutokana na kukabiliana na maneno mengi kwa kukosa mtoto.

Wema amesema kuwa picha zinazoonekana zimetengenezwa na si zake kama inavyozungumzwa mitaani.

Hata hivyo baada ya kuziona hata yeye zimemliza, lakini wazo la mtu aliyezitengeneza picha hizo zinaweza kuumba ukweli wa mawazo yake.

"Aliyetengeneza hiyo picha kajua kuniliza, ila hata mawazo huumba ukweli. Jamani naulizwa sana na watu kama ni mjamzito, jibu ni hapana wapenzi... Ila tuzidi kuomba Mungu... Inshallah," aliandika Wema.

Wiki mbili zilizopita Wema Sepetu alitokwa na machozi ya furaha na kuonyesha shukrani na faraja yake kwa watu waliomwandikia jumbe kwenye chapisho la picha alizopakia akisherehekea siku ya kuzaliwa kwa binti wa mpenzi wake Whozu.

Lola ambaye ni mtoto wa Whozu na Tunda alikuwa anasherehekea kufikisha umri wa miaka miwili, na Wema alisimama kama mama kwa mtoto huyo kusherehekea pamoja na Whozu.

**BASI SAWA**

## Shakila kafa kaoza




MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Lavalava, ametambulisha kipande cha ngoma yake mpya ambayo mrembo kutoka Kenya Shakila, atakuwa amepamba video yake.

Katika video hiyo ameonekana Shakila akiwa amemlalia mwanamuziki huyo kifuani, huku LavaLava akiwa kwenye usingizi mzito.

Mrembo huyo kutoka Kenya ni maarufu katika mitandao ya kijamii na kushiriki kwake inaongeza hamasa ndani ya lebo ya WBC ambayo wasanii wake wanapenda kupamba video zao na warembo kutoka nchini humo.

## Young Lunya afanya yake



RAPA Young Killer Msodokii, ameonyesha umwamba wake baada ya kuwakimbiza wasanii wakubwa katika chati ya nyimbo zinazofanya vizuri katika mitandao ya kijamii.

Kupitia wimbo wake mpya wa Freestyle Session 6, msanii huyo ameendelea kushika nafasi ya kwanza katika mtandao wa You tube, kama wimbo unaofanya vizuri zaidi nchini.

Mwanamuziki huyo ameshika nafasi hiyo baada ya kuishusha 'My Baby' ya Diamond Platnumz, huku Freestyle Session 5 ya Young Lunya ikiwa namba tatu.



# HAMISA NANI KAFANYA YOTE

SWALI ambalo bado halijajibiwa ni nani yuko nyuma ya mafanikio ya malkia wa mitindo, Hamisa Mobetto, kiasi cha kununua gari jipya la kifahari aina ya Range Rover Velar?

Kitendawili cha mtu anayehusika na mambo yote bado hakijateguliwa, lakini kwa sasa ni habari ya mjini ni Hamisa, kuposti video fupi akionekana akiwa ndani ya ndege binafsi na kisha kwenda kuliona gari hilo la kibabe.

Katika miandao ya kijamii, baadhi ya watu wamezidi kutoa maoni yao na wengine kuhisi msanii huyo wa Bongo Fleva amepata mwanaume mwenye fedha zake ambaye anagharamia mambo yote kwa sasa.



# Diamond sasa umeshindikana

WENGI wamepigwa na butwaa baada ya staa wa muziki wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz, kuonekana akiwa na mrembo kwenye kochi huku wakivaa nusu utupu.

Kipande hicho ambacho kinaonekana ni sehemu ya wimbo wake mpya, imewashtua mashabiki wengi wa muziki na kuhoji pengine kuna uhalisia nje ya kazi na mrembo huyo.

Baadhi ya watu waliotoa maoni wameeleza jinsi video hiyo ilivyowapagawisha na kueleza endapo wimbo huo ukitoka hewani, Diamond atakuwa na stori nyingine juu ya mrembo huyo kutokana na tabia yake ya kubadilisha wanawake.

**FILAMU**

# Chozi la Mama: Halidondoki bure

**Na Adam Fungamwango**

MAMA ni mama, mama hana mfano na akifa hakuna mwingine atakupenda kama yeye. Ni baadhi ya mashairi kutoka kwa wimbo wa Dr. Remmy aliwasifia wanawake.

Ni kweli kabisa, duniani hakuna kama mama. Binadamu anaweza kufanyia watu mambo wengi mazuri, lakini hali inapokuwa mbaya kwake mama yake ndiyo anaubeba uchungu wote.

Mwanaume anaweza kupata pesa nyingi anatumia na warembo wote wa dunia, lakini anapoumwa wote watamkimbia. Ni mama yake tu ambaye hatomkimbia, tena inawezekana atakuwa hakufaidi matunda yoyote ya mwanawe.

Maana yake ni kwamba utakimbiwa na wanawake wote lakini siyo mama.

Kwa maana hiyo kila mtu anatakiwa amheshimu na kumpa kipaumbele sana mama yake kwanza kabla ya watu wengine kama alivyofanya mwamba mwenye filamu hii.

"Chozi la Mama' ndiyo filamu yenyewe ambayo imechezwa na Fikiri Salum kama Tom, Lapi Dat akicheza kama Lipi, Ramadhani Mwambe yeye ni Wakutengwa, Nikras Mapenda akitumia jina na Mogaji, Nasra Mpemba kacheza kama Mpemba, Rose Kawaga akicheza kama Mkenya, Zubeda Hamza, Bi Zuki, Neema Mussa akitumia jina la Nay, Salma yeye ni Salma.

Tom anaota ndoto mbaya inayomhusu mama yake huko kijijini. Akaamua aende na kumkuta yupo hoi, anaumwa.

Akaamua amlete mjini kwa ajili ya kumpa matibabu sahihi na kumuuguza.

Bi Zuki anapata uangalizi mzuri kutoka wa mkwewe Lipi kiasi cha kujiona kama vile yupo peponi licha ya ugonjwa wake. Alikuwa amenoa. Tamaa, binti mmoja kwenye nyumba hiyo ya kupanga na mwenzake wanashawishi Lipi amtese mama wa watu.

Wakamwambia mama huyo anamfanya kama mtumwa au hausigeli wake. Lipi akabadilika. Akambadilikia mama mkwe wake. Akaanza kumtesa. Akamnyima chakula na kumfanyia kila aina ya dhihaka. Kwa bahati mbaya sana Tom yeye anafanya kazi za kusafiri hivyo muda mrefu anakuwa hayupo nyumbani.

Inafika wakati sasa baadhi ya majirani wenye huruma ndiyo wanaompa chakula Bi Zuki. Tom anarejea kutoka safari na kukuta habari mbaya kuhusu mama yake na mkewe.

Anamtimua mkewe. Anachukua panga kwenda kwa Tamaa kwa lengo la kumdhuru kwa madai ameiharibu nyumba yake.

Hata hivyo mama yake akamkalisha chini na kumshauri asifanye jambo lolote baya kwa yoyote yule. Lipi anakwenda kwa shaangazi yake Tom kumuangukia naye anamrudisha kwa mumewe kwa lengo la kumuombea msamaha. Shangazi yake alishirikiana na mama yake wanamshawishi Tom amsamehe mkewe kwa madai kuwa dunia imeshamfunza.



## WANAIMBA LAIVU BILA CD

**Na Adam Fungamwango**

KUMEKUWA na wasanii wengi nchini ambao wanasaidiwa mno na 'maprodyuza', huku wenyewe wakiwa hawawezi kupiga muziki laivu.

Wasanii wengi wa Watanzania ukitaka kuwaweza, kuwe na muziki wa laivu na piga hata nyimbo zao zile zile kwa vyombo, halafu waambie waende kuimba, utashangaa.

Unaweza kudhani kuwa siyo yule aliyeimba ngoma hiyo. Ukweli ni kwamba wasanii wengi wanaingia studio kwenda kuimba tu. Tena wakati mwingine wanaimba vibaya, lakini wasaidiwa na prodyuza na makompyuta yake.

Halafu mirindimo inatafutwa na prodyuza. Msanii anakuja kuishtukia ngoma yake tayari imeisha huku kila kitu akiwa amefanyiwa.

Lakini kuna watu huwa wanapiga nyimbo za wasanii kwa kutumia vyombo halisi vya muziki. Sasa mwite msanii mwenyewe aliyeimba wimbo huo apande jukwaani, anashindwa kuimba kama vile alivyorekodi studio.

Ni kwa sababu kule alikuwa anarudia sana. Sauti imerekebishwa na vitu vingi vya kiufundi.

Ukweli ni kwamba wana matatizo ya 'key', yaani ufunguo. Hata ngoma yake mwenyewe anakuwa hajui ameimba key gani.

Ataimba kwa sauti ya juu sana kuliko vyombo vinavyopigwa au chini na kusababisha wimbo kutokuwa kwenye hali yake ya kawaida.

Wana matatizo pia ya 'timing'. Kujua hapa ndipo pa kuingilia kuimba na hata pa kutokea.

Ndiyo maana baadhi ya wasanii wakajiongeza na kuanza kujifunza kupiga muziki laivu.

Hawa ukiwapigia nyimbo zao kwa kutumia magitaa, wataimba tu hawana wasiwasi wowote hata ukiwaamsha usiku wa manane.

Leo tunawataja wasanii ambao ni kama wanamuziki tu, wana uwezo mkubwa wa kuimba muziki wa 'laivu' bila matatizo.

**Lady Jaydee**

Ni msanii mkongwe nchini ambaye kwa sasa unaweza kabisa kumwita ni mwanamuziki.

Katikati ya miaka ya 2000 alipokwenda nchini Uingereza na kina King Kiki na marehemu Ndala Kasheba, alikutana na changamoto ambayo ilimfanya kuanza kujifunza kupiga muziki laivu.

Ni kwamba wakongwe kina King Kiki ndiyo waliokubaliwa zaidi kwa sababu walipiga muziki laivu na wao walikuwa wanatumia 'play back' yaani CD. Wazungu walikuwa wapenzi wa hilo. Wao walitaka muziki wa laivu. Mwanamuziki Oliver Mtukudzi kutoka Zimbabwe ambaye naye alikuwa huko, ndiye aliyemshauri Lady Jaydee kupiga muziki wa laivu kwa sababu ana uwezo mkubwa wa sauti nzuri. Aliporejea alinunua vyombo na kuunda bendi yake ya Machozi. Kwa sasa anaimba laivu kama kawaida.

**Banana Zorro**

Unaweza usishangae sana kwa sababu huyu ni mtoto wa mwanamuziki Zahir Ally Zoro aliyepigia bendi za JKT Mafinga, maarufu kama Kimulimuli, Sambulumaa na nyingine nyingi.

Alijiingiza kwenye muziki wa kizazi kipya, lakini yeye akiwa na uwezo mkubwa wa kuimba laivu akipigiwa vyombo. Pia anajua kupiga gitaa, hivyo ni mwanamuziki aliyekamilika.

**Ali Kiba**

Katika hali inayoonyesha kuwa jamaa ni mbishi na pia ana kipaji halisi cha muziki, Ali Kiba ni mmoja wa wasanii mwenye uwezo mkubwa wa kuimba laivu. Kuna baadhi ya matamasha yake, nyimbo zake nyingi amekuwa akiziimba huku akiwa anapigiwa magitaa na vinanda na kuziimba vile vile kama zilivyorekodiwa studio, kitu ambacho ni ngumu mno kwa wasanii wengi ambao amekuwa tu akishika 'mic', na kusema yo yoo, nyimbo zao zikipigwa 'play back', yaani zile zile walizorekodi studio.

**Peter Msechu**

Huyu pia ni mmoja wa wasanii ambao wana uwezo na ujuzi mkubwa wa kusimama jukwaani na kuimba muziki wa laivu bila matatizo yoyote na amekuwa akifanya hivyo siku zote.



# Tanasha huyo mwamba nani?

MWANAMUZIKI kutoka Kenya, Tanasha Donna, amesababisha mjadala katika mitandao ya kijamii baada ya kuweka picha ya mwanamume mmoja anayedhaniwa kuwa mpenzi wake raia wa Nigeria.

Kwenye picha Tanasha akiwa amemwagia makopakopa mwanamume huyo huku akisema kuwa asingeweza kuwa na subira zaidi kama hajamwona, maneno ambayo jamaa huyo alimjibu kwa mahaba huku akimtaja waziwazi kama mpenzi wake.

Sasa story zinaendelea na kiki za hapa na pale baada ya mwanamuziki huyo kuonekana kwenye video ya wimbo wa msanii wa Nigeria, Lojay unaokwenda kwa jina Ova ambapo hajashirikishwa kama mwimbaji bali ameshiriki kama video vixen.

Tanasha hivi sasa anahusishwa sana na kuwa na mahusiano na mwanaume wa Nigeria japo yeye hajathibitisha kwani ni miaka mingi tangu kuachana na baba wa mtoto wake, msanii Diamond pLatnumz kutoka hapa Tanzania.



# Jamie Foxx kuandaa filamu ya Vandross

KULINGANA na taarifa kutoka Hollywood, mwigizaji Jamie Foxx, yuko mbioni kutengeneza filamu inayohusu maisha ya rapa Luther Vandross na atasaidiwa na kuhusisha kampuni.

"Luther ni mmoja wa waimbaji wakubwa katika historia ya muziki. Kwa kweli ni heshima kuwa sehemu ya timu kusaidia kuleta hadithi hii ya kushangaza kwa watu," alisema.

Hadithi inayotengeneza filamu hiyo inatokana na kitabu pekee cha wasifu wa Vandross, 'Luther: The Life and Longing of Luther Vandross', ambacho kiliandikwa na mwanahabari mkongwe wa muziki Craig Seymour.

# LL Cool J ataja kuanza ziara

RAPA mkongwe nchini Marekani, LL COOL J, hatimaye ametangaza tarehe ya kuanza ziara yake yaliyoitwa 'F.O.R.C.E. Tour', baada ya kuiahirisha mara kadhaa.

Ziara hiyo ambayo itakuwa na mastaa kibao inaanzia Agosti 11 katika mji wa Baltmore na kubalizika Novemba 19 katika Jiji la Boston.

"Lazima niwape mashabiki wangu uzoefu ambao hauwezi kusahaulika, nataka kuhakikisha kuwa kila kitu kimefanywa sawa, na ili kufanya hivyo, ilibidi nibadilishe mambo kadhaa."

"Umewahi kufanya ziara za uwanjani hapo awali aliulizwa akajibu, nimefanya ziara za uwanjani hapo awali. Lakini sijawahi kuhisi kama zilikuwa zangu," alisema LL Cool J.





# Duh! Kisicho riziki, hakiliki

MWIMBAJI kutoka mtaani mwenye utata, Habeeb Olawunmi, maarufu kama Portable, aliponea chupuchupu kufa baada ya kupata ajali mbaya wakati akiendesha gari lake jipya aina ya G-Wagon.

Katika video mpya inayosambaa katika miktandao, inaonyesha gari hilo la kifahari likionekana limepondeka pondeka.

Taarifa zinaeleza lilitokea huko Osapa London, Lekki, Jumatano alipokuwa akipelekwa kwenye studio yake ya muziki wakati mvua kubwa ikinyesha.

# Cynthia hatunaye tena

MWIGIZAJI mkongwe wa Nigeria Cynthia Okereke, ameaga dunia.

Kupitia ukurasa wa Twitter wa msanii mwenzake, Joseph Okechukwu, alieleza Cynthia alifariki Jumanne akiwa hospitalini akipatiwa matibabu.

"Nimevunjika moyo kupita maneno, ukweli kwamba nilikuwa naenda kulipia tiketi yako ya ndege ili nije kumaliza tulichoanza tu, kusikia ulienda kwa Mungu, ni mojawapo ya mambo magumu ambayo nimewahi kushughulika nayo katika siku za hivi karibuni."

Ameandika Okechukwu.



# Kiwanda chaagizwa ajira kwa wazawa

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

SERIKALI imeielekeza menejimenti ya Kiwanda cha Mbolea cha Itracom kutoa kipaumbele cha ajira kwa wazawa zaidi badala ya kufikiria kuajiri idadi kubwa ya wafanyakazi kutoka nje ya mkoa wa Manyara.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, aliagiza jana kipaumbele kuzingatiwa ili kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana waliomaliza vyuo vya kati na vyuo vya elimu ya juu.

"Mkoa wa Manyara una wasomi ambao hawana ajira rasmi mkitaka wataalamu tangaza ajira wazi ili watu waombe kazi," alisema Sendiga.

Aidha, alisema kwa mamenejа watakaopangiwa kufanya kazi mkoa huo waangalie wazawa ndio wawapikie na siyo na kuja na watu wa kuwapikia mameneja na wazawa wakakosa ajira.

"Kuwapa fursa wazawa ni kutengeneza ulinzi kiwanda hicho ambacho kitakuwa mkombozi kwa wananchi," alisema.

Mkuu huyo wa mkoa pia aliagiza Serikali ya Kijiji cha Vilima Vitatu na Halmashauri ya Wilaya ya Babati, kupanda miti ya vivuli shuleni hapo, maua na miti mingine.

"Muwafuate TFS (Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania) ili mpewe miti ya kutosha mpande hapa, ambayo haina gharama yoyote," alisema.

Sendiga alielekeza uongozi wa shule hiyo kuhakikisha wanafunzi wanakuwa na madawati ya kutosha wasikae chini kwa kuwa kukaa chini ni hatari kwa afya yao kutokana na kuwapo kwa marumaru madarasani.

Akijibu agizo hilo la Mkuu wa Mkoa, Mwenyekiti wa Bodi ya Itracom, Kapteni mstaafu John Chiligati, alisema kiwanda kikikamilika kitaajiri watu 1,000.

Alisema kazi zisizohitaji ujuzi, wazawa wa kijiji cha Vilima Vitatu ndio watapewa kipaumbele.

Kuhusu uwekezaji wenye tija, Chiligati alisema wataleta mtambo wa kuzalisha tani 200,000 za mbolea.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda hicho, Kimaramzilo Nkurikiye, alisema wametumia Sh. bilioni 6.500 kujenga shule hiyo na kuweka miundombinu ya shule ili watoto waweze kusoma vizuri.

Akitoa shukrani kwa serikali kufikia shuleni hapo, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Vilima Vitatu, Denis Mtui, alisema shule hiyo ilianza mwaka 1968 ina wanafunzi.

# Mil. 942/- kutekeleza miradi ujenzi wa madarasa, mabweni, nyumba ya mwalimu

**Na Allan Isack,** ARUMERU

SERIKALI imetoa Sh. milioni 942.2 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mitatu ya maendeleo kwenye sekta ya elimu kwa shule za sekondari za halmashauri ya Arusha.

Fedha hizo ni za Mradi wa Kuboresha Elimu kwa Shule za Sekondari (SEQUIP).

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, alisema jana kuwa serikali imetoa fedha hizo kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya elimu kwa shule za sekondari.

Alisema Sh. milioni 584.2 zitatumika kujenga shule mpya ya sekondari katika Kata ya Moivo na Sh.milioni 260 zitakuwa za ujenzi wa mabweni na ukarabati katika Shule ya Sekondari ya Mringa.

Aidha, mkurugenzi huyo alisema Sh. milioni 98 zitatumika kujenga nyumba moja ya walimu yenye sehemu ya kuishi familia mbili kwenye Shule ya Sekondari ya Kiutu.

Lengo lengo la serikali kutoa fedha hizo, alisema ni kuboresha miundombinu ya shule za sekondari ili kupandisha kiwango cha elimu nchini.

Katika taarifa yake, Msumi alisema dhamira ya serikali kutoa fedha za utekelezaji wa miradi hiyo ni kuhakikisha wanafunzi wanasoma katika mazingira salama, ikiwamo mazingira ya kufundishia kwa walimu na kujifunzia kwa wanafunzi.

"Tunaishukuru serikali yetu kwa kutupatia fedha hizi kwa kuwa zitakuwa na msaada mkubwa, hasa ukarabati na kuboresha miundombinu ya elimu kwa shule zetu za sekondari.

"Fedha hizi zitakuwa na umuhimu kwa kuwa zitasaidia kuweka mazingira mazuri na rafiki kwa walimu wakati wakifundisha na wanafunzi wakijifunza darasani," alisema.

Pia alisema miradi hiyo, itatekelezwa kwa muda wa miezi mitatu kwa kutumia utaratibu uliowekwa na serikali wa kuwatumia mafundi jamii yaani 'Force Account'.

"Katika utekelezaji wa miradi tutatumia 'Force Akaunti' kwa kuwa ni utaratibu uliowekwa na serikali na miradi itajengwa kwa ubora na kutakuwapo kwa matumizi sahihi ya fedha kulingana na thamani ya mradi," alisisitiza Msumi.



Diwani wa Kata ya Endiamtu, Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, Lucas Zacharia, akizungumzia kero na changamoto za miundombinu ya elimu kwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, alipofanya ziara ya kutembelea kata hiyo, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# RC apiga 'stop' watendaji kata, vijiji kuingilia vyombo vya watumiaji wa maji

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, amesema kuanzia sasa ni marufuku watendaji wa kata na vijiji kuingilia vyombo vya watumia maji katika utendaji kazi wao, kwa kuwa kufanya hivyo ni kuzuia taasisi zinazotakiwa kujiendesha zenyewe.

Alitangaza marufuku hiyo jana, wakati akikabidhi vifaa kwa viongozi wa vyombo vya watumia maji kwa Wilaya zote za mkoa huo.

Vifaa hivyo vimetolewa na Wakala wa Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira (RUWASA) Mkoa wa Manyara.

"Vyombo vya watumia maji viachwe vifanye shughuli zake. Watendaji wa kata, vijiji na wenyeviti wasiwaingilie wawaache wafanye hesabu zao," alisema Sendiga. Hoja kuhusu vyombo hivyo kuingiliwa majukumu yao iliibuliwa na Meneja wa Vyombo vya Watumia Maji kutoka RUWASA Makao Makuu, Valentina Masanja.

Kutokana na tatizo hilo, pia Sendiga ameagiza wakurugenzi wa halmashauri na wenyeviti kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo la kukosekana ofisi huku akisisitiza kuwa lazima watoe ardhi ya ujenzi wa ofisi hizo.

"Hawa wana bajeti zao siyo watawaomba watatumia fedha zao kujenga ofisi watapata maeneo yao na kujenga ili watunze vizuri vifaa vyao," alisema Sendiga. Naye Masanja alisema vyombo hivyo vimeundwa kwa mujibu wa sheria, hivyo ni vizuri visimame katika nafasi zao.

Alisema makusanyo wanayopata ni kwa ajili ya kuendeleza upatikanaji wa huduma na siyo vinginevyo.

Masanja alisema si jukumu la serikali kuwanunulia vifaa bali wao inabidi wanunue kutoka kwenye mapato yao.

Awali, Meneja wa RUWASA Mkoa wa Manyara, Walter Kirita, alisema RUWASA ina hudumia asilimia 85 ya wananchi wote. Kwa mujibu wa Kirita, ili kuboresha huduma za maji kwa mwaka wa fedha 2023/2024 zimetengwa Sh. bilioni 5 kuanzisha miradi mipya na Sh. milioni 765 kuchimba visima kwa kutumia mafundi jamii yaani "Force account".

TULIKOTOKA, TULIKO & TUNAKOKWENDA

# Enzi za misuko 'tatu kichwa', 'twende kilioni'

Na Adam Fungamwango



UKIPITA sehemu mbalimbali nchini, mijini na vijijini siku hizi kuna saluni. Za kike na za kiume. Kusambaa kwa umeme sehemu nyingi za nchi na hata maeneo mengi jijini Dar es Salaam, kumesababisha kuwepo kwa saluni nyingi nchini. Na hii imesababisha ajira kwa baadhi ya vijana.

Zamani mpaka katikati ya miaka ya 1990, hata kwenye jiji kubwa kama la Dar es Salaam usingeweza kukuta umeme kwenye nyumba nyingi. Nyumba zilizokuwa na umeme zilihesabika.

Labda kwenye nyumba ambazo zilikuwa na maduka. Na hata baadhi yao ziliweka taa aina ya karabai ambazo zilikuwa zinawaka mithili ya taa za umeme. Kwa sasa karabai si nyingi sana.

Mikoani na vijijini ndiyo kabisa. Umeme ilikuwa ni hadithi ya kufikirika. Mpaka mjini, tena kwenye majengo machache ya serikali.

Kutokana kutosambaa sana kwa umeme miaka ya nyuma, watoto wengi, vijana na hawa watu wazima walikuwa wanakwenda kunyoa nywele zao sehemu fulani ambazo zilikuwa maarufu sana wakati huo.

Ni chini ya mti. Saluni zilikuwa ni chini ya miti mikubwa. Waliokuwa wananyoa wengi wao walikuwa watu wazima kwa umri. Walikuwa wanatumia mikasi na wembe.

Hakukuwa na ulazima ya mti fulani utumike, bali mti wowote mkubwa ambao unatoa kivuli ulikuwa unatumika kama saluni au ofisi za kunyoa.

Chini ya mti utakuta viti kadhaa za mbao, na meza ambazo inakuwa imeegemezwa katikati ya mti.

Kioo kikubwa nacho kinakuwa imefungwa kwenye mti na kuning'inia.

Watoto wa miaka 1970, 1980 na hata 1990, watakumbuka jinsi walivyokuwa wakipelekwa kwenye saluni hizo za kienyeji, ingawa wakati huo tulikuwa hatuiti saluni bali kwa kinyozi.

Wakifika hapo wanavingirishwa nguo nyeupe na kuwekwa kwenye kiti, tayari kwa kunyolewa na mkasi, wakati mwingine ikichanganyika na wembe.

Tatizo kwenye baadhi ya timu hasa miembe kulikuwa na wadudu aina ya washawasha ambao walikuwa wanaleta usumbufu mkubwa.

Na mara nyingi watoto walipelekwa siku chache kabla ya sikukuu, au kabla ya kufungua shule. Vinginevyo, baba mwenyewe, mama anaweza akamalizika na wewe nyumbani.

Twende kwa upande wa akinadada nao pia hawakuwa na saluni pia. Wao walikuwa wanasukana wenyewe kwa wenyewe.

Mama mmoja alikuwa anaweza kutoka nyumbani kwake na kwenda kwa jirani na kuomba asukwe.

Kama nafasi ipo wakati huo atasukwa, lakini kama hakuna atapewa ahadi baadaye, kesho au siku nyingine.

Wanawake walikuwa wakisukana bure kabisa. Labda ni kwa sababu wakati huo bado Watanzania walikuwa wanaishi kijamaa. Sikuwahi kuona hata siku moja mwanamke akimsuka mwenzake akalipwa kama ilivyo hivi sasa.

Wakati wa kusukana sasa. Mmoja atakaa chini, iwe chini kabisa au kwenye mkeka. Msukaji atakaa kwenye kiti na shanuo. Hiki ndicho kinatumika kufumua nywele zilizozipo, au kuzichana kwamba kabla ya kusukwa.

Wanawake wakati huo walitumia kuanzia dakika 30, mpaka masaa mawili kutengemea na aina ya nywele zenyewe zinazusukwa.

Mitindo iliyotikisa sana wakati huo miaka ya 1970, 1980 hadi mwanzoni mwa 1990 ni 'vitunguu', 'twende kilioni', 'uti wa roda', 'jicho la mke mwenza', 'mabutu', 'kilimanjaro' na mingine mingi.

Hii ilikuwa ni kabla ya saluni kuanza kuelenea kutokana na mabadiliko ya teknolojia, hasa baada ya umeme kusambaa.

Kabla ya hapo, tayari baadhi ya wanawake ambao walianza kujipambanua kuwa ni wa kisasa wakati ule, walikuwa wameshaanza kwenda mbali sana na kuchoma nywele zao.

Walikuwa wanatumia vitana vya chuma kuweka kwenye moto na baadaye kuzipitisha kwenye nywele.

Mtindo huu ulianza kuwa maarufu sana katikati ya miaka 1990 hadi mwanzoni mwa miaka ya 2000, ambapo telnolojia iliendelea kukua mno, badala ya kuzichoma, sasa zilikuwa zinawekwa kwenye mashine.

Wanawake waliochoma nywele, na kupaka dawa za kuzifanya nywele kuwa nyeusi zaidi maarufu kama zazuu, walionekana warembo mno kutokana na kwamba ilikuwa haijazoeleka kuwaona wasichana au wanawake wakiwa kwenye muonekano huo.

**Tuma meseji 0716 350534**



# Utafutaji wa mkaa unavyobeba simulizi za 'kufa na kupona' porini

INATOKA UK. 4

**BAADA YA PORINI**

Seif anatanguliza hoja kwamba bidhaa hiyo ina soko kubwa. Namna wanavyoipata porini, wananunua mkaa kwa bei ya jumla Sh. 120,000 kwa magunia matatu na wanayauza kwa Sh. 320,000.

"Wateja ni wengi sana, wanasimama barabarani wanatusimamisha, lakini soko kuu la mkaa ambalo bodaboda wote wanauza ni Mbezi kwa Njemba njia ya kwenda Goba, Mbezi kwa Yusuph na sehemu nyingine ni Kibanda cha Mkaa na (Mbezi), sehemu nyingine ni kuzia mtaani, maeneo ya Kifuru, Maramba Mawili, hadi Gongo la Mboto," anakutaja kote mkoani Dar es Salaam.

Seif anadokeza siri ya pikipiki zao kuwa na uwezo wa ziada katika kubeba mzigo wa mkaa, kwamba zinafanyiwa marekebisho ya kiufundi, 'shokapu' zake zinaboreshwa kwa kuinuliwa, vilevile eneo la nyumba kunakobebwa mzigo.

Pia anaeleza vipindi linganifu vya kisheria dhidi ya biashara ya mkaa, akifafanua kuwa kuna wakati serikali ilikuwa imetoa rukhsa kwa bishaara ya mkaa, watu walikuwa wanalipa ushuru na anakiri kwa kutumia tathmini yake kwamba "ajali zilipungua" kwa kundi lao.

Anapofananisha ushuhuda binafsi wa mazingira, alipotakiwa kutoa tathmini yake, Seif anakiri hali ni mbaya, misitu inatoweka kwa kasi, akitumia mfano wa miaka mitatu pekee - eneo la Ruvu, misitu inatoweka kwa kasi kutokana na uchomaji mkaa.

Pia anataja Kitongoji cha Kwala anakoishi, kuelekea umbali wa kilomita 15 ambako kuna pori, nalo uchomaji mkaa unalipa hali mbaya.

**MAISHA MAPYA**

Seif anasema kuwa baada ya kuacha kufanya kazi hiyo, alijaribu kuwashawishi wenzake kuachana na shughuli hiyo yenye kuteketeza misitu, huku akiwapa mbinu kujikita katika biashara ndogo au ufugaji wa kuku wa kienyeji kama ambavyo anafanya yeye.

Anataja ushauri mwingine aliowapa ni kuunganisha nguvu na kukodisha gari na kwenda kubeba mkaa kwa sababu magari yameruhusiwa kwa kibali maalum.

"Katika kundi letu la watu 40, wapo walionisikiliza na kuachana na kazi hiyo, ingawa suala la kukodi gari limekuwa gumu kutokana na kipato kidogo.

"Hii niliiangalia kutokana na familia inayotufuata nyuma, kwani tunakuwa kwenye hatari kubwa sana ya kuziacha ama



Waziri January Makamba.



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu.

yatima au tegemezi kutokana na madhila ambayo tunakumbana nayo ikiwamo kifo na ulemavu wa kudumu," anasema.

**MATUMIZI YA GESI**

Rose Fantael, mkazi wa Mbezi Kibanda cha Mkaa mkoani Dar es Salaam, aliyekuwa akitumia mkaa ambao upatikanaji wake unahusisha mbinu hatari zilizotolewa ufafanuzi na Seif, anasema alitawaliwa na imani kwamba bidhaa hiyo ni nafuu kuliko nishati ya gesi.

"Zamani nilikuwa ninaamini mkaa ni nafuu kuliko gesi, kumbe sio kweli. Nimeacha kutumia mkaa, ni muda sasa ninatumia gesi nyumbani kwangu na nimenunua jiko lake kabisa. Sasa ninapika kwa haraka na chakula kinakuwa kitamu tu," Rose anasema.

Rose anajibu dhana ya walio wengi kuwa matumizi ya mkaa katika mapishi ni bora, ambapo sasa anakiri kuokoa fedha nyingi zilizotumika kununua mkaa. Sasa ana faida nyingine - anatumia muda mfupi zaidi kupika kwa kutumia nishati safi (gesi).

Anabainisha kuwa awali alikuwa anatumia gunia moja la mkaa kwa mwezi mmoja kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Ana familia ya watu wanane.

"Gunia la mkaa nilikuwa ninanunua Sh. 38,000, tunalitumia mwezi mmoja limeisha. Kwa sasa ninatumia gesi kilo 15 ninajaza kwa Sh. 50,000, ninatumia kwa miezi miwili au zaidi. Sasa, ukilinganisha gharama za mkaa na gesi unaona kabisa gesi ni mkombozi," anasema.

**MKAANGA CHIPSI**

Emmanuel Kipeta, mkazi wa Mbezi kwa Yusuph mkoani Dar es Salaam, anasema elimu inatakiwa kutolewa kuhusu gharama ya nishati safi ya kupikia (gesi) na matumizi yake kwa kuwa wengi wana hofu huhusu hilo pamoja na wasiwasi wa usalama wao pindi ajali itakapotokea.

Kipate, ambaye ni mfanyabiashara wa kukaanga viazi (chipsi), anasema katika biashara yake anatumia mkaa na ziada ya kuni na maranda yanayotokana mbao zilizorandwa.

"Mimi kwa siku ninatumia gunia moja la mkaa hadi mawili ambayo ninanunua Sh. 33,000, hapo wakati mwingine ninanunua hadi Sh. 40,000, lakini nikiwaza kutumia gesi ninaona itakuwa gharama kubwa sana ukizingatia sokoni vitu vimepanda bei sana," anasema.

Kipate anasema anajua kutumia mkaa ni uteketezaji misitu. Anakiri kama angekuwa na ufahamu kuhusu matumizi ya gesi na faida zake angehamia huko kwa kuwa anachokitafuta ni faida katika biashara yake.

**TFS, WHO**

Mnamo tarehe 3 Septemba 2019, Mkurugenzi wa Idara ya Misitu wa TFS, Arjanson Mloge, alikaririwa akisema mahitaji makubwa ya mkaa yametengeneza soko kubwa jijini Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya, Dodoma na miji mingine.

Mloge alisema mkaa unaoingia Dar es Salaam ni magunia 500,000 kwa mwezi, akirejea utafiti uliofanywa na TFS kati ya Desemba, 2016 na Januari, 2017.

"Kiasi hiki hakijumuishi mkaa unaoingizwa isivyo halali na bodaboda zinazokisiwa kuwa takribani 200 kwa siku. Mikoa inayoingiza kwa wingi mkaa jijini Dar es Salaam ni Pwani, Tanga, Morogoro, Njombe (miti ya kupandwa), Lindi na Mtwara," Mloge alibainisha.

Shirika la Afya Duniani (WHO) duniani tayari limeshaonya kupitia ripoti yake ya utafiti ya mwaka jana kwamba, moshi unaotokana na kuni za kupikia ni mojawapo ya visababishi vikuu vya vifo vya watoto wachanga duniani, ukigharimu maisha ya watoto 500,000 wenye umri chini ya miaka mitano kila mwaka.

Utafiti huo unachambua matumizi ya nishati hizo na kuenea kwa magonjwa ya kupumua kwa watoto hao kupitia utafiti uliofanywa katika nchi 30 zinazoendelea kutoka mabara ya Asia, Afrika na Amerika ya Kusini.

Matokeo yalipendekeza jamii kuweka nje majiko yanayotumia nishati hizo. Utafiti ulibaini watu bilioni tatu katika nchi zinazoendelea wanategemea kuni au mkaa kwa ajili ya kupikia.

Kwa mujibu wa WHO, magonjwa yanayosababishwa na moshi husababisha vifo vya watu milioni 4.3 kila mwaka, vikiyapiku magonjwa ya malaria na kifua kikuu (TB).

**HATUA SERIKALINI**

January Makamba, Waziri wa Nishati, anaeleza mabadiliko ya tabianchi, kwa kiasi kikubwa yanachangiwa na uharibifu wa mazingira, ikiwamo ukataji miti kwa ajili ya kuni na mkaa.

"Uharibifu wa mazingira pamoja na mambo mengine, unatokana na matumizi ya vyanzo vya nishati visivyo rafiki wa mazingira," anatamka, January akiwa na msisitizo wa kipaumbele vijijini kuwe na nishati safi kwa gharama nafuu, akihimiza iendane na ustawi wa wanawake katika eneo hilo.

Waziri huyo anatoa historia kwamba Novemba mwaka jana, wizara yake iliandaa Mjadala wa Kitaifa wa Nishati Safi ya Kupikia, wa kuibua vikwazo vilivyopo katika lengo hilo, huku ukipanua wigo wa kupatikana teknolojia na nishati safi ya kupikia nchini.

Ni mjadala uliozinduliwa na mwasisi wa hoja, Rais Samia Suluhu Hassan, aliyeagiza kuundwa kwa Kikosi Kazi cha Kitaifa kitakachoandaa Dira ya Kitaifa ya Nishati Safi ya Kupikia, kuakikisha asilimia 80 ya Watanzania wanahamia katika nishati safi ya kupikia ndani ya miaka 10 ijayo, huku akitaka kwa kila taasisi za umma na binafsi zinazokusanya zaidi ya watu 300, kuanzia Januari mwakani, waachane na matumizi ya kuni na mkaa.

Kwa mujibu wa Waziri January, hadi sasa kimeshaundwa kikosi kazi husika kitaifa kinachojumuisha ngazi za wizara na taasisi zake, chini ya uratibu mkuu wa Wizara ya Nishati, huku kukiwapo kamati ya mawaziri inayoandaa dira, ambazo ni: Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) na Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu).

Zingine ni: Wizara ya Fedha, Wizara ya Nishati, Wizara ya Madini, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Afya, pamoja na wadau wa sekta binafsi, asasi zisizokuwa za kiserikali na washirika wa maendeleo.

Kwa mujibu wa January, unatekelezwa mijini katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Mwanza, Pwani, Tanga na Tabora unafadhiliwa na Jumuiya ya Ulaya (EU) kwa thamani ya Euro milioni 30.

Waziri anasema serikali kupitia Mradi wa Umeme Vijijini (REA), inaendelea kutekeleza programu inayowezesha kupatikana nishati safi ya kupikia na katika mchango wake, REA inawezesha usambazaji na kupatikana mitungi bora ya gesi kutoka sekta binafsi.

**JICHO LA KITAALAMU**

Kunatajwa kuwapo athari za kiafya kwa wazalishaji na watumiaji wa mkaa kwa kuwa una kemikali ya kaboni, ambayo inapochomwa ina hatari ya kuchafua afya ya mtu aliyeko jirani, kupitia uchafu kama masizi yanayoingia na hewa kirahisi ndani ya mapafu.

Mtaalamu wa magonjwa ya upumuaji, Dk. Elisha Osati, anasema kuni na mkaa zina kawaida ya kutoa chembe ndogo zinazoweza kupenya katika njia ya hewa, hata kusababisha athari kiafya.

Dk. Osati anafafanua kwamba, hewa anayoiita kitaalamu 'kaboni monoksaidi', inayotolewa na mkaa, pia kuni, inapoingia mwilini inapenya katika damu na kuanzisha athari ya kuondoa hewa ya Oksijeni, ambayo ni muhimu kwa uhai wa mtu na ndio unakuwa mwanzo wa madhara ya muda mfupi na mrefu.

Dk. Osati anadokeza adha mojawapo ya kuni na mkaa kwa mtumiaji - moyo wake kushindwa kufanya kazi.

Anaendelea kufafanua: "Uchomaji wa mkaa unaweza pia kusababisha matatizo ya kupumua na hatimaye kupata maambukizi ya njia ya hewa (ARI), ugonjwa sugu wa mapafu (COPD), pumu, saratani ya mapafu au kwa wajawazito kujifungua watoto wenye uzito wa chini."

**MITUNGI NAFUU**

Simulizi ya magumu hayo, inapata ufafanuzi wa mbadala nafuu wa kuondosha kuni na mkaa sokoni kwa kukaribisha gesi unaowapa fursa hata wenye kipato cha chini kunufaika nayo.

Mkurugenzi wa Taifa Gas, Hamis Ramadhan, anasema katika kuwezesha wigo mpana wa watumiaji wa nishati hiyo mbadala, ni vyema wasambazaji wake wakawezesha zikapatikana kwa gharama nafuu.

Ramadhan, katika maoni yake anaamini huo ni mbadala na wakati huo huo unaendana na kipato cha wengi, hata kuipatia sifa ya kusaidia kuhamasisha matumizi ya gesi majumbani na kwingineko.

"Mitungi ya kilo tatu sasa hivi ipo, bei yake kujaza ni Sh. 13,000 na kimsingi inapendwa na inatumiwa na watu wengi. Mitungi ya kilo mbili iko mbioni, tuna uhakika wasambazaji wenzetu wa gesi wanaliangalia hilo suala, tutakwenda mpaka pale kiwango cha chini ya kujaza kitaruhusiwa kitendaji," anahitimisha Ramadhan, ambaye taasisi yake pia ni mdau wa mstari wa mbele kuhamasisha mageuzi hayo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KIWANJA KINAUZWA

**KIWANJA KIPO KISUKURU** SEGEREA **JKT DSM,** KINA UKUBWA WA MITA ZA MRABA **(SQM) 2252,** KIWANJA KIMEPIMWA KINA HATI, **BEI MILIONI 60.** KWA MAWASILIANO: **0754 857523, 0655857523**

---

JAMHURI YA MUUNGANO TANZANIA
KUITWA SHAURINI MDAIWA
(MCA)
Mahakama ya Mwanzo ya ARUSHA MJINI
Wilaya ya ARUSHA
TALAKA NAMBARI…YA …20
Mdai WINIFRIDA GUSTAKI SHAYO
amdai
Mdaiwa HUMPHREY WILFRED MASSAWE
Kwa. HUMPHREY WILFRED MASSAWE WA KISONGO

Kwa kuwa Mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba (eleza hapa habari za madai)

Kuja kujibu madai ya talaka, mgawanyo wa mali na matunzo ya watoto
Unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria mahakama hii siku ya jumanne tarehe 18/07/2023 saa 2.30 asubuhi/alasiri kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Angalia kama hukuhudhuria/ hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 13/7/2023

Hakimu / Hakimu Mkazi/Mahakama ya Mwanzo

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
WILAYA YA KILOSA
S.L.P.29
KILOSA
YAH:MAOMBI NA. 47/ 2014
ABDALLAH MOHAMED SULUMWA: ……MLETA MAOMBI
VERSUS
SALEHE ABDALLAH SALUMU:…………MJIBU MAOMBI
SALEHE OMARI SHAWEJI:………………MJIBU MAOMBI

WITO/KUITWA SHAURINI

KWA
SALEHE OMARI SHAWEJI
POPOTE ULIPO Unaarifiwa Ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Kilosa, tarehe 17/07/2023 wewe mwenyewe au mwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kusikilizwa.
Endapo hamtahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.
Imesainiwa leo tarehe 11mwezi 04 Mwaka 2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
KILOSA

---

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 77 OF 2023
IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE REV. JONAS PETRO MKOBA of Dodoma City
AND
IN THE MATTER OF THE APPLICATIONFOR LETTERS OF ADMINISTRATION OF A SMALL ESTATE BY AGNES JONAS MKOBA

GENERAL CITATION
(Rule 75)
ALL PERSONS Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Admirations made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before 2 Day of 8, 2023.
Dated at Dodoma this 14 day of 7, 2023

RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA DISTRICT

---

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

HABIBU RAMADHAN ISMAIL Anatangaza kupotelewa kwa kadi tatu za piki piki zenye namba za usajili MC 434CTG/MC 291 DJS/MC 877DRK (haojue) ,Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu nayeye. MOR/MOR/RB/236535/2023.

---

IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF RUNGWE DISTRICT
AT KIKUYU
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 05 OF 2023
IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE MELANIA MREMA KYANDO
AND
LILIAN HILLARY MREMA…………1ST APPLICANT
HAPPY HILLARY MREMA…………2ND APPLICANT.

GENERAL CITATION
(Made under rule 75)

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate ( or letter of administration) is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filled on or before the 18th day of AUGUST, 2023
Dated at Rungwe this 14th day of JULY, 2023

DISTIRCT RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE
RUNGWE - TUKUYU

---

KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA
SONGEA LILILOKO SONGEA
MAOMBI NAMBA 53/2023
**JOSEPH LAURENT TOLLE ——– MUOMBAJI**
DHIDI YA
**ABDU NASSORO TOLLE ——–MJIBU MAOMBI**
**ELVIS JOSEPH HULUKA——— MJIBU MAOMBI**

WITO /KUITWA SHAURINI
Wajibu maombi mnataarifiwa kuwa muombaji amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yenu .Hivyo basi mnatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au wakili wenu ,au wote kwa pamoja siku ya tarehe 11/08/2023 saa 2.00 asubuhi.Kumbuka pia nyaraka zote kuhusu mgogoro huu zipo hapa barazani kwa ajili ya kuleta hati zote zenu za utetezi.
Kumbuka pia kushindwa kwenu kufika shaurini kutapelekea baraza hili kusikiliza shauri hili upande mmoja bila kujali uwepo wenu.
Imetolewa leo nami na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 14/07/203.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
SONGEA

---

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 74 OF 2023
IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE SAMWELY JORAM MGULLOH of Dodoma City
AND
IN THE MATTER OF THE APPLICATIONFOR LETTERS OF ADMINISTRATION OF A SMALL ESTATE BY MIRIAM SAMWELY PETER
GENERAL CITATION
(Rule 75)

ALL PERSONS Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Admirations made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before 18 Day of 7, 2023.
Dated at Dodoma this 14 day of 7, 2023

RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA DISTRICT

---

SHAURI JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya ………..TANGA
Kituo cha MJINI TANGA………..Mkoa TANGA
Usimamizi wa mirathi Na...125.../2023
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU: PETER MNYAMBUMGAYA
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI
YALIYOLETWA NA: STELLA PETER MGAYA
TANGAZO
(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)
Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo tarehe 20 mwezi 7 mwaka 2023 kabla, huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
*Marehemu hakuacha wosia
Imetolewa leoTarehe ….13… mwezi …7…mwaka 2023

HAKIMU

---

OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.
Mobile: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz,
Website: www.ippmedia.com

---

# OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

# MOB: +255 - 0677020701

# E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,

# WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, kiungo vya mwili wa bianadamu vilianguka. Majirani kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Kinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

## MAITI KWENYE KIROBA-17

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

***MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, kiungo vya mwili wa bianadamu vilianguka. Majirani kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Kinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.***

****************************************

Maria aliondoka taratibu akirudi ofisini huku akigeuka mara kwa mara kumtazama Eddy.

Alipohakikisha Maria ameondoka alitoka taratibu kwenda sehemu ambayo taxi huwa zinapaki.

Alikwenda hapo kwa nia moja tu, kuisaka ile taxi aliyoiona kwenye video aliyotumiwa na Maria. Namba alikuwa ameshaziandika kwenye mkono wake wa kushoto. Kwa mbinu za hali ya juu hakuonekana kama analitafuta.

Mwishoni alidhani labda limeshaondoka kupeleka abiria mahali fulani. Wakati akiwa amekata tamaa akaiona taxi yenye namba hiyo. Akaifuata taratibu. Mlangoni alikuwa dereva. Bahati iliyoje, kwani ni yule yule aliyembeba jamaa aliyeshuka kwenye ndege kutoka Mwanza siku ya mauaji ya Tessy.

Kile kibegi chake kilionekana kama na yeye ni msafiri fulani hivi. Muda mfupi uliopita ilitua ndege kutoka Zanzibar. Alionekana kama mmoja wao.




**"Rudisha uso wako mbele, haraka sana." Haikuwa sauti ile waliyokuwa wanaongea habari za Simba na Yanga.**

"Karibu bwana." Akakaribishwa.

"Ahsante sana, nataka unipeleke Kawe."

"Kawe gani?"

"Mzimuni."

Wakati akijibu hivyo, tayari alikuwa mlango wa nyuma wa gari, akifungua. Hakutaka kukaa mbele kwa makusudi. Ni kwa sababu ya kazi ambayo anataka kuifanya.

Dereva hakuwa na hofu yoyote ingawa si mara nyingi wateja hupenda kukaa nyuma. Ni mara chache sana hasa wale waliojifanya mabosi sana. Lakini abiria wengi hupenda kukaa mbele. Huyu aliyempata alikuwa mmoja kati ya abiria wachache wanaopenda kukaa siti ya nyuma.

Kama ilivyokuwa kwa mpelelezi aliyekuhubu kama yeye, alitafuta kitu chochote ambacho kingemfanya dereva huyo kuwa rafiki badala ya dereva na abiria wake.

Aliona gazeti la michezo likiwa limepachikwa chini ya kioo cha mbele cha gari. Hakupoteza muda.

"Kiongozi naomba hilo gazeti." Aliomba kwa sauti ya kirafiki.

Hakujibu kitu, aliachia usukani mkono wa kushoto akabaki ameushikilia kwa mkono wa kulia. akanyoosha mkono kuchukua gazeti, akaukunja kwa nyuma kumpatia.

"Ahsante." Akashukuru huku akipokea.

"Unajua nilivyokuona sikudhani kama wewe ni shabiki wa mpira." Dereva alianzisha mazungumzo.

Ilikuwa ni turufu kwa Eddy kwani alikuwa anatafuta njia ya kutaka kuongea naye na ndiyo maana alianza kwa kuomba gazeti.

"Sana tu, mimi ni mpenzi wa soka."

"Unapenda timu gani?"

"Hapa au nje ya nchi?"

"Hapa nchini, mimi mwenzako ni Yanga."

"Okay, mimi pia kama wewe ni Yanga." Eddy akaongopa. Hajawahi kuwa Yanga hata siku moja. Ni shabiki wa Simba, lakini aliona ajibu hivyo ili dereva afurahi kuwa kumbe abiria wake pia ni shabiki timu yake. Hakutaka kuanza kuulizana maswali, kutaniana ana kucharurana, alichotaka wazungumze lugha moja. Ndege wa rangi moja huruka pamoja siku zote.

"Safi kabisa, nje mimi ni Arsenal." Dereva alizidi kumjulisha abiria wake.

Eddy hakutaka kurudia tena kusema ni shabiki wa Arsenal. Alihofia kuonekana huenda haongei sahihi.

"Huko mwana mimi sina timu. Mimi kila anapokwenda kocha Jose Mourinho ndiyo huko huko na mimi napenda.

Alipokuwa Chelsea, akaenda Inter Milan, Manchester United, Tottenham Hotspur na sasa yupo Roma, kote huko mimi namfuata tu, sasa hivi ni shabiki kindakindaki wa Roma."

Jibu hilo lilimchekesha sana dereva, halafu akaishia kusema "Du! Rafiki yangu wewe kiboko."

Waliendelea kuongea mengi hasa ikiwa ni harakati za usajili kwa klabu yao zinazoendelea na mambo mbalimbali yahusuyo klabu yao na mafanikio makubwa waliyoyapata msimu uliopita, kuchukua Ngao ya Hisani, Ubingwa wa Ligi Kuu, Kombe la FA na kufika Fainali ya Kombe la Shirikisho Barani Afrika.

Kwa bahati nzuri Eddy alijua vitu vingi kuhusu michezo, hivyo alimfurahisha sana dereva japo ukweli hakuna Yanga.

Ilitimu saa tatu kasorobo usiku, gari ilikuwa imepita maeneo ya Lugalo na sasa ilikata kona kulia kuelekea Kawe.

Kabla ya kufika maeneo ya Kawe Ukwamani sehemu ambayo kulikuwa na miti miti hivi na majani, Eddy akamuomba dereva akaweke gari pembeni ili akajisaidie."

Hakuwa na hiana, akafanya hivyo tena huku akiendelea kupiga stori ikionekana kama wameshazoena na stori za michezo zimenoga.

Alifikiria kuwa mlango ungefunguliwa ili abiria wake atoke kujisaidia. Haikuwa hivyo. Badala yake akasikia bega likiguswa kwa nguvu kidogo.

Alichodhani ni kwamba abiria wake ameshindwa kufungua mlango, hivyo aligeuza sura ili ahakikishe kama ndivyo hivyo kabla hajapekeleka mkono wake nyuma kumfungulia.

Alichokiona hakuamini. Ni kama alikuwa anaota ndoto ya jinamizi. Alichokishuhdia ni mdomo wa bastola iiyokuwa imeelekewa kichwani.

"Rudisha uso wako mbele, haraka sana." Haikuwa sauti ile waliyokuwa wanaongea habari za Simba na Yanga.

Ni kama aliyeongea ni mtu mwingine sana. Hali hiyo ilimtisha dereva. Alirudisha sura yake mbele.

"Nyoosha mikono juu." Aliamriwa na kutii.

"Mimi ni mtu mzuri sana, wala sina haja ya kukudhuru, na wala si nia yangu. Ninachotaka unijibu maswali yangu machache tu, ukinijibu kwa ufasaha bila uongo au hadaa nitakuachia urudi nyumbani uendelee na maisha na familia yako. Lakini kama ukiniongopea na kunisumbua, nitatanya ubongo wako."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# DODOMA JIJI KUSAJILI SABA WAPYA, YAMTAJA MTENJE

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI imefanikiwa kumnasa kiungo mkabaji wa Coastal Union, Albano Mtenje, Klabu ya Dodoma Jiji imesema itasajili wachezaji wapya saba ili kuimarisha kikosi chake kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakafanyika kuanzia Agosti 15, mwaka huu.

Mtenje anatajwa pia alikuwa anawindwa na Simba ili kuziba nafasi iliyoachwa na kiungo mzawa, Jonas Mkude.

Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili ya Dodoma Jiji, Fredrick Mwakisambwe, alisema wamefanikiwa pia kuwabakisha wachezaji wao muhimu 20 ambao walipambana kuibakisha timu hiyo katika msimu uliopita.

**Mwakisambwe alisema usajili wao utazingatia zaidi ya maeneo ambayo yameainishwa na Kocha Mkuu wa timu hiyo, Melis Medo.**

"Tumeanza rasmi usajili wetu hususan kwa wachezaji ambao wanatoka nje ya timu, kwa maana ya wageni, tumeshamsajili Mtenje kutoka Coastal Union, pasipo na shaka ni mmoja wa wachezaji bora katika nchi yetu, tunatarajia atakuja kuongeza kitu kikubwa sana ndani ya timu yetu kwenye eneo la kiungo wa uzuiaji," alisema Mwakisambwe.

Aliongeza baada ya kukamilisha usajili wa mchezaji huyo, sasa wako katika hatua za mwisho za kuongeza nyota wengine sita ambao watakiongezea nguvu kikosi hicho kilichomaliza katika nafasi ya tisa msimu uliomalizika.

"Kuna wachezaji wengine sita ambao tutawasajili, wale wachezaji walioipambania timu hadi ikabaki na ambao tulikuwa tuna mipango ya kuendelea nao wote wamebaki kwa kuwaongeza mikataba, kusema kweli kikosi chetu hakitakuwa na mabadiliko makubwa sana," Mwakisambwe alisema.

Mwenyekiti huyo alisema lengo la usajili huo ni kutengeneza kikosi kitakachokuwa na ushindani na kuondokana na wasiwasi wa kushuka daraja kama waliokuwa nao kwa misimu miwili iliyopita.



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Karate ya wanawake wakifanya mazoezi kujiandaa na mashindano ya Maziwa Makuu yatakayofanyika hivi karibuni nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Azam yaisubiri US Monastir

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI wachezaji wa Azam FC wameahidi kupambana kuhakikisha wanafanya vyema katika msimu ujao, uongozi wa timu hiyo umesema wameomba mchezo wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya US Monastir ya Tunisia.

Azam imeweka kambi yake Tunisia na pia imepeleka maombi kwa klabu nyingine za nchini humo, CS Sfaxien na Esperance.

Mchezaji mpya wa timu hiyo, Djibril Sillah, alisema anaamini msimu ujao watafanya vyema lakini ameshangazwa na ubora wa nyota aliowakuta katika kikosi hicho na kutamba wanaweza kushinda kombe lolote.

"Nimeungana na timu, ninachokiona nimevutiwa sana na uwezo wa wachezaji, nafikiri tuna timu nzuri sana kwa sababu wachezaji wote wana ari na uwezo mkubwa, nafikiri msimu ujao unaweza kuwa na tofauti tunaweza kushinda kombe kwa sababu wachezaji wote ni wazuri sana," alisema kiungo huyo mshambuliaji, raia wa Gambia aliyesajiliwa akitokea Raja Casablanca ya Morocco.

Naye Abdul Suleiman Sopu, alisema amevutiwa na mazoezi ya kocha wao mpya na kueleza anawapa vitu vipya ambavyo hawajawahi kuvipata.

"Yaani ukiniambia nimwelezee kocha wetu huyu mpya sijui nianzie wapi, yaani vitu tulivyokutana navyo sio mchezo, nasema msimu ujao unaweza kuwa mzuri kwetu," alisema Sopu.

Ofisa Habari Msaidizi wa timu hiyo, Hasheem Ibwe, alisema wanasubiri majibu kuhusu mechi za kirafiki walizoomba dhidi ya timu wenyeji za hapo Tunisia.




## Malale kubakia JKT Tanzania

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa JKT Tanzania umesema unaendelea kumwamini kocha wake, Hamsini Malale, kwa ajili ya kukinoa kikosi cha timu hiyo iliyorejea katika Ligi Kuu Bara itakayoanza rasmi ifikapo Agosti 15, mwaka huu.

Tayari JKT Tanzania imeshakamilisha usajili wa wachezaji wapya akiwamo Said Ndemla kutoka Mtibwa Sugar, Hassan Dilunga (Simba), Ismail Aziz Kader (Azam FC) na Deusdedith Okoyo aliyekuwa anaichezea Geita Gold FC.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa JKT Tanzania, Speratus Lubinga, alisema kwa sasa hawafikirii kufanya mabadiliko yoyote katika benchi lao la ufundi.

"Tuna mipango ya muda mrefu na Kocha Malale, kwa sababu amefanikisha malengo yetu kwa asilimia kubwa, hatuwezi kumwondoa, tunaimani naye ataendelea kuwapo katika benchi la ufundi kwa ajili ya kuendeleza safari yetu ya matuamini mazuri katika Ligi Kuu Bara msimu wa 2023/24," alisema Lubinga.

Kikosi cha JKT Tanzania tayari kimeingia kambini Dodoma kwa ajili ya maandalizi ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya Kombe la FA.

## Tanzania karate kuchuana Congo

**Na Abdallah Mataka**

TIMU ya Taifa ya Karate inatarajia kushiriki katika mashindano ya kimataifa ya Maziwa Makuu yatakayofanyika kuanzia Julai 17 hadi 23, mwaka huu Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), imefahamika.

Rais wa Shirikisho la Karate Nchini, Yahya Mgeni, aliliambia gazeti hili maandalizi ya kikosi cha Tanzania yanaendelea vizuri na jumla ya wachezaji 20 kutoka mikoa mbalimbali wanaunda timu hiyo.

Mgeni alisema mashindano hayo yatafanyika kwa michezo yote ya kata na komite.

"Tunaye kocha kutoka Burundi ambaye anafundisha komite lakini pia tunaye, Seiss Ahmadi kutoka Nigeria kwa ajili ya upande wa kata, tumejipanga kutokana na ukubwa wa mashindano hayo, ninaahidi Watanzania wategemee timu yao inakwenda kufanya vizuri kama tulivyofanya mwaka 2021," alisema Mgeni.

Nahodha wa timu hiyo, Petro Madai, alisema wamejiandaa vizuri ili kuhakikisha wanakwenda kupeperusha vyema bendera ya Tanzania na kuutangaza mchezo wa karate.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

**MAHREZ ANUKIA ARABUNI**
KLABU ya Al Ahli inatayarisha dau la pauni milioni 30 kwa ajili ya kumnunua winga wa Timu ya Taifa ya Algeria, Riyad Mahrez, mwenye umri wa miaka 32 kutoka Manchester City. (*Athletic*)

**GUARDIOLA, MAHREZ KUTETA**
KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola anatazamiwa kufanya mazungumzo na Riyad Mahrez kutokana na nia iliyoonyeshwa na klabu hiyo ya Saudi Arabia. {*Mirror*)

**FABINHO ATAJWA SAUDIA**
KLABU ya Saudi Arabia ya Al-Ittihad iko tayari kutoa ofa ya pauni milioni 40 kwa ajili ya kumnunua kiungo wa kati wa Liverpool, Fabinho mwenye umri wa miaka 29, ambaye ni raia wa Brazil. *(Athletic*)

**HENDERSON AWEKWA SOKONI**
KIUNGO wa kati wa Liverpool na England, Jordan Henderson, mwenye umri wa miaka 33, amekubali mkataba mnono kutoka kwa klabu inayonolewa na Steven Gerrard ya Al-Ettifaq. *(Guardian)*

**ALCANTARA KUREJEA BARCA**
KIUNGO wa kati wa Liverpool na Timu ya Taifa ya Hispania, Thiago Alcantara, mwenye umri wa miaka 32 anaweza kurejea Barcelona msimu huu wa joto. (*Sport*)

**LATIA ANUKIA LIVERPOOL**
LIVERPOOL huenda wakamnunua kiungo wa kati wa Southampton na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Romeo Lavia, mwenye umri wa miaka 19. (*Mirror*)

**VILLA YAMTAKA DIABY**
KLABU ya Aston Villa imewasilisha ombi lao la kwanza la kumnunua winga wa Bayer Leverkusen mwenye umri wa miaka 24, Moussa Diaby. (*Sky Sports Germany*)

**ONANA SAFI UNITED**
MANCHESTER United inakaribia kufikia makubaliano yenye thamani ya pauni miloni 43, pamoja na nyongeza ya pauni milioni 4.3 kwa mlinda mlango wa Inter Milan, ambaye ni raia wa Cameroon, Andre Onana, mwenye umri wa miaka 27. *(Fabrizio Romano)*


**SPURS KUMBAKISHA KANE**
KLABU ya Tottenham Hotspur itampa mshambuliaji wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 29, mkataba mpya utakaomfanya alipwe mshahara wa pauni 400,000 kwa wiki, huku kukiwa na nia kutoka Bayern Munich. (*Telegraph)*

**HOJLUND MAMBO MAGUMU**
OFA za mchezaji wa Manchester United pamoja na fedha kwa mshambuliaji wa Denmark, Rasmus Hojlund mwenye umri wa miaka 20, zimekataliwa na Atalanta, ambao wanataka malipo kamili ya fedha. (*Athletic*)

**TRINDADE SOKONI EPL**
KLABU ya Fulham ina matumaini ya kuzishinda Barcelona, Atletico Madrid, Arsenal na Liverpool hadi kufikia makubaliano ya kumnunua kiungo wa kati wa Fluminense na Brazil, Andre Trindade, mwenye umri wa miaka 21. *(90min*)

**SANGARE AKARIBIA FOREST**
KLABU ya Nottingham Forest iko katika mazungumzo ya juu zaidi ya kumsajili kiungo wa kati wa Ivory Coast, Ibrahim Sangare, mwenye umri wa miaka 25 kwa mkataba wa pauni milioni 30 kutoka PSV Eindhoven. (*Football Insider*)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# LIVERPOOL YAFIKIRIA HATIMA YA FABINHO

**LIVERPOOL,** England

●●● Ni baada ya klabu hiyo kupokea ofa kutoka kwa mabingwa wa Ligi Kuu ya Saudia...

LIVERPOOL inaifikiria ofa kutoka kwa mabingwa wa Ligi Kuu Saudi Arabia, Al Ittihad kwa ajili ya Fabinho, vyanzo vimeiambia 90min.

**Wekundu hao wanaimarisha safu yao ya kiungo, huku tayari wakiwa wamewasajili Alexis Mac Allister na Dominik Szoboszlai katika dirisha hili la joto.**

90min iliripoti Alhamisi, Jordan Henderson pia anawaniwa na Al Ittihad, ambayo inanolewa na gwiji wa zamani wa Liverpool, Steven Gerrard.

Thiago Alcantara amekataa ofa ya kujiunga na Saudi Pro League kipindi hiki cha majira ya joto, na sasa kiungo wa tatu wa Liverpool anawindwa na miamba hiyo kutoka Mashariki ya Kati.

90min inaelewa wakati Liverpool haina mpango wa kupoteza viungo wengi kipindi hiki cha majira ya joto, wanafikiria kama wanaweza kumuuza Fabinho kwenda Al Ittihad baada ya kupokea ofa.

Mabingwa hao wa Saudia tayari wamemsajili, Karim Benzema, N'Golo Kante na Jota, sasa wanamtaka Fabinho kujiunga nao.

Kikosi hicho cha Kocha, Jurgen Klopp kipo kwenye heka heka ya kuimarisha nafasi yao ya kiungo huku nyota wa Southampton, Romeo Lavia na Ryan Gravenberch wa Bayern Munich wakiwa kwenye rada zao.

Kiwango cha Fabinho hakikuwa cha kuridhisha wakati wa msimu mbaya wa Liverpool wa 2022/23, wakimaliza nafasi ya tano kwenye Ligi Kuu England huku wakitolewa mapema kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Nyota huyo wa Brazil alijiunga na Liverpool kutoka Monaco kwa ada ya awali ya pauni milioni 39 na ameshinda kila mashindano akiwana wekundu hao.

HABARI MICHEZO

# Pulisic rasmi asajiliwa AC Milan

**MILAN,** Italia

KLABU ya AC Milan inayoshiriki Ligi Kuu Italia maarufu Serie A imekamilisha usajili wa Christian Pulisic kutoka Chelsea kwa kupewa mkataba wa miaka minne, huku kukiwa na kipengele cha nyongeza ya mwaka mmoja.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 ameondoka katika Ligi Kuu England baada ya miaka minne, ambako alicheza mechi 145 katika mashindano yote na alitwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2021.

"Ninafuraha kubwa kuwa hapa. Nimehamasika. Nimehamasika kuanza kuichezea klabu hii yenye historia," alisema Pulisic.

"Nipo tayari kuwa hapa na kujaribu kushinda mataji nikiwa na klabu hii.

"Naamini nilikuwa na wakati mzuri kule Chelsea. Nilijifunza mengi kama mchezaji na nimekua vya kutosha, lakini sasa nimekamilika kwa ajili ya kuichezea AC Milan," aliongeza.

"Nakumbuka nilicheza hapa kwenye Uwanja wa San Siro katika Ligi ya Mabingwa Ulaya na sikuamini nilichokiona kabla ya mchezo wakati mashabiki walipokuwa wakishangilia na kupiga kelele.

"Hali ya hewa hapa ni ya kuvutia. Sikuwahi kupata uzoefu kama ule. Nafikiri AC Milan, ikicheza kwenye San Siro, pengine ni sehemu bora sana duniani kwa mechi kubwa."

Fowadi huyo ametoka kwenye msimu mbaya wa 2022/23, akifunga bao moja na asisti moja kwenye mechi 24 akiwa Chelsea.






# GERRARD AMTAKA MANE KUMFUATA SAUDI ARABIA

**MUNICH,** Ujerumani

MSHAMBULIAJI wa Bayern Munich, Sadio Mane, anawindwa na timu inayoshiriki Ligi Kuu ya Saudi Arabia, Al Ettifaq, ambayo inanolewa na gwiji wa Liverpool, Steven Gerrard, kwa mujibu wa 90min.

Mane ambaye ameacha alama pale Anfield aliondoka Merseyside na kujiunga na miamba ya Bavaria kipindi cha majira ya joto kilichopita baada ya miaka sita ya mafanikio kwa wekundu hao.

Alitarajiwa kuwa na mafanikio makubwa kule Allianz Arena wakati Bayern Munich ikishinda taji lake la 11 mfululizo kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, lakini hakuwa katika kiwango bora na akawa kwenye mgogoro mkubwa baada ya kugombana na Leroy Sane kuelekea mwisho wa msimu.

Katika mechi 38 alizocheza kwenye mashindano yote, Mane alifunga mabao 12 na kutoa asisti sita kwa Bayern Munich.

90min iliripoti mwezi uliopita, Mane alikuwa anatakiwa na Waarabu, lakini yeye hakuwa na mpango wowote wa kuhamia mashariki ya kati.

Hata hiyo, 90min sasa inaelewa Bayern Munich inajaribu kumuuza Mane na wanaona Saudi Arabia ndio sehemu wanayoweza kupata ofa kubwa.

Al Ettifaq, ambayo hivi karibuni ilimteua Gerrard kuwa kocha wake mpya inataka pia kumsajili nahodha wa Liverpool, Jordan Henderson, na sasa inamtaka Mane ambaye anawaniwa na Al Ahli, Al Ittihad, Al Hilal na Al Nassr, zote za Saudi Arabia.

# Ten Hag kuamua nahodha United

**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag amesisitiza kikosi cha Manchester United hakitasaidia kuamua nani atakuwa nahodha mpya msimu ujao.

Nahodha wa sasa wa Wekundu hao, Harry Maguire, amekuwa na wakati mgumu chini ya Ten Hag, akianza kwenye mechi nane tu za Ligi Kuu msimu uliomalizika.

Kukosa nafasi ya kucheza mara kwa mara sasa kumemfanya nahodha huyo kuwa kwenye uwezekano wa kuondoka hapo Old Trafford.

90min iliripoti mapema kipindi hiki cha majira ya joto, Tottenham Hotspur imemtaja mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, huku Juventus, Inter, Newcastle United na West Ham United zote zikionyesha nia ya kumhitaji mchezaji huyo.

Licha ya klabu nyingi kumtaka, vyanzo vimebainisha Maguire anataka kubakia United ili kupigania nafasi yake.

Wakati wa kukosekana kwa Maguire, Bruno Fernandes alikuwa nahodha namba moja wa kikosi hicho, huku Raphael Varane aliiongoza kwenye mchezo wa ushindi wa kujiandaa na msimu mpya dhidi ya Leeds United mjini Oslo Jumatano.

Akizungumza kuhusu nani atakuwa nahodha wa kikosi hicho msimu ujao, Ten Hag alibainisha haitaamuliwa na kikosi, lakini kocha mwenyewe.

"Hapana, sitaamua wachezaji wachague. Ni juu yangu mimi," alisema.



## HABARI MICHEZO

# ROBERTINHO AITAKA TATU BORA AFRIKA MSIMU UJAO

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Mbrazil Roberto Oliveira 'Robertinho', amesema anatamani kuona kikosi chake kinawapata wachezaji wote wapya wanaowahitaji ili kumaliza msimu ujao katika nafasi ya tatu kwenye ubora Afrika.

Robertinho ametoa kauli hiyo kutokana na baadhi ya nyota wapya waliosajiliwa katika kikosi hicho kushindwa kuripoti kambini kwa wakati huku timu hiyo ikiwa imeshaanza kambi yake nchini Uturuki.

Moja ya nyota anayesubiriwa kikosini hapo ni winga, Luis Miquissone, ambaye usajili wake bado haujakamilika mpaka kufikia jana jioni.

Kwa sasa mabosi wa Simba wanakamilisha taratibu za safari kwa nyota wake wapya ambao ni Willy Onana, Che Fondoh Malone, Jean Baleke na Fabrice Ngoma aliyetambulishwa jana ili kuelekea Uturuki hapo keshokutwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Robertinho alisema msimu ujao wanatarajia kushiriki mashindano mengi ikiwamo Super League ambayo ni muhimu kufanya usajili mzuri utakaowapeleka kufikia malengo yao.

Robertinho alisema Simba itakutana na timu kubwa katika michuano hiyo mipya, hivyo wanahitaji kuimarisha kikosi ili kuipeperusha vyema bendera yake lakini ikifanya vyema kwenye Ligi Kuu Bara.

"Usajili ni mzuri na wachezaji wenye kiwango kizuri ambao watafikia malengo yao, Simba iko ndani ya 10 bora katika viwango vya Fifa ni jambo la kujivunia hii inatokana na uwezo mkubwa wa wachezaji wazuri na kufanya vizuri katika michuano.

Sasa tunahitaji wachezaji wazuri jambo ambalo linafanyiwa kazi na viongozi wangu, wanakamilisha usajili na kujiunga na timu kwa ajili ya maandalizi yetu ya msimu ujao," alisema Robertinho.

Aliongeza Simba inaendelea na programu ya mazoezi kwa awamu mbili (asubuhi na jioni) huku akifurahia mazingira mazuri ya kambi ambayo yanaongeza umakini.

"Mazoezi ya asubuhi yalikuwa mapesi kwa ajili ya wachezaji kuweka miili sawa, zoezi hili likisimamiwa na kocha wa viungo (Corneille Hategekimana), walianza kukimbia nusu uwanja kabla ya kuanza ya viungo ikiwamo kutumia vifaa mbalimbali kama fimbo fupi za kuruka na koni na mazoezi ya jioni yanakuwa ya nguvu," alisema kocha huyo.

Naye Mratibu wa Simba, Abbas Ally, alisema kambi hiyo inaendelea vizuri na wachezaji wengine walitarajia kuwasili nchini humo leo.

Alisema hadi kufikia Julai 20, mwaka huu wachezaji wote ambao wamesajiliwa na Simba kwa ajili ya msimu ujao watakuwa wameungana na wenzao kwa ajili ya kukamilisha maandalizi ya kuelekea msimu mpya.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussen Ali Mwinyi (wa pili kulia), akiangalia mazingaombwe kutoka kwa msanii, Issa Juma Issa wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), kwenye kilele cha Maonyesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Yanga: Tumemnasa 'Mbappe wa Congo'

INATOKA UK 24

"Niseme tu sisi tumekwenda kuboresha kikosi chetu, tuna wachezaji wazuri sana kwenye eneo la pembeni, tunachofanya ni kuboresha na kuongeza changamoto ya upinzani uwe mzuri, pia tuwe na upana wa kikosi kwa maana ya viwango vya wachezaji visipishane sana," Kamwe alisema.

Aliongeza baada ya kumnasa Nzengeli, watakamilisha usajili wa nyota wa kigeni kwa mchezaji ambaye atakabidhiwa jezi na sita.

Aliwataja pia mashabiki wa Yanga waendelee kuvuta subira kwa sababu wiki ijayo ndio watawapa furaha zaidi kwa 'kushusha kifaa' hatari zaidi.

"Wachezaji waliotambulishwa akiwamo Mkude tayari wameingia kambini, wanaendelea na programu za mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya wakiwa chini ya kocha mpya (Miguel Angel Gamondi)," aliongeza ofisa huyo.

Kuhusu kauli ya Simba ya kutaka kumwalika Mkude katika Tamasha la Simba Day kwa ajili ya kumwaga kutokana na kazi kubwa aliyoifanyia klabu hiyo kwa miaka 13 mfululizo, Kamwe alisema hilo hawataruhusu.

"Labda watafute Mkude mwingine wamuage, kama shida ni kuaga lakini siyo huyu, ila kama wanaona ni lazima wafanye hivyo basi tunawaalika wao waje Siku ya Mwananchi ili wamuage," alisema Kamwe.

# Pambano la Dulla, Katompa layeyuka

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Abdallah Pazi maarufu Dulla Mbabe amesema hawezi kupanda ulingoni kupambana dhidi ya Mkenya Denzel Onyango badala ya Erick Katompa, kama ilivyotarajiwa hapo awali.

Dulla Mbabe alibadilishiwa mpinzani baada ya Katompa kushindwa kutokea katika zoezi la kupima uzito lililofanyika jana jijini Dar es Salaam.

Akizungumza jijini jana, Dulla Mbabe, alisema amesikitika kuona amepangiwa bondia mwingine ambaye hamfahamu.

"Mimi sikujipanga kupigana na Onyango, nimefanya mazoezi ya muda mrefu kwa ajili ya Katompa, kwa upande wangu huu ndio uamuzi wangu, ni hayo labda uongozi wangu ukae kwa ajili ya kutoa tamko," alisema bondia huyo.

"Tunaomba radhi Watanzania kwa changamoto iliyotokea, bondia wangu alipata majeraha ya goti wakati tulipokuwa tunafanya mazoezi ya mwisho hivyo hawezi kuwapo kesho (leo)," alisema Lewis Mulamba, Kocha wa Katompa.

Naye Rais wa Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa Tanzania (TPBRC), Chaurembo Palasa, alisema suala ambalo limejitokeza kutokana na changamoto ni la kawaida katika mchezo huo.

Mratibu Mkuu wa PeakTime Media Presents, Selemani Semunyu, alisema Katompa ameshindwa kufika kutokana na changamoto ya usafiri.

Semunyu alisema Onyango amemzidi uzito Dulla Mbabe, hivyo watakaa kuzungumza na bondia huyo ili kufanya mchakato wa kupunguza uzito lakini akiwataka mashabiki wajitokeze kwa wingi katika pambano hilo.

# Ngoma mali ya Simba SC

INATOKA UK 24


karibia kukamilisha mazungumzo na mchezaji wanayemtaka kwenye nafasi hiyo.

Simba ndio timu pekee kutoka Afrika Mashariki na Kati itakayoshiriki mashindano mapya ya Super League yatakayofanyika kuanzia Oktoba 20, mwaka huu na uzinduzi wake utafanyika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kwa sasa kikosi cha Simba kiko Uturuki na wachezaji wake waliobakia nchini kwa ajili ya kukamilisha taratibu za safari, wanatarajia kuondoka jijini Jumatatu.

Mnyama ataanza msimu mpya kwa kucheza dhidi ya Singida Fountain Gate katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya Ngao ya Jamii wakati mabingwa watetezi wa taji hilo watakutana na Azam FC, mechi zote zikichezwa kwenye Uwanja wa CCM, Mkwakwani, Tanga.

**Michezo**
**Nipashe** Jumamosi Julai 15, 2023



UK. 21

## Liverpool yafikiria hatima ya Fabinho




Kiungo mpya wa Simba ambaye ni raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Fabrice Ngoma, kutoka Al Hilal ya Sudan. **PICHA: SIMBA SC**

## Yanga: Tumemnasa 'Mbappe wa Congo'

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

MABINGWA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wamesema wamefurahishwa na usajili wa winga Mkongomani, Maxi Mpia Nzengeli (23), akitokea Maniema United, ambaye wanamfananisha na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Kylian Mbappe.

Hata hivyo Yanga imesema haitakuwa radhi kumpa ruhusa kiungo wao mpya, Jonas Mkude, kuagwa na timu yake ya zamani, Simba.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema viongozi wa klabu hiyo hawakufanya kosa kwenda Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), kumsajili Nzengeli kwa sababu mchezaji huyo ana uwezo mkubwa wa kucheza nafasi za pembeni na kati, akijaaliwa nguvu za kupiga mashuti makali, kutoa pasi za mwisho na kufunga akiwa amepachikwa jina la Mbappe.

Yanga ilimtambulisha rasmi mchezaji huyo aliyepewa mkataba wa miaka miwili juzi usiku, akiwa ndiye mchezaji wa pili wa kigeni, nyota wengine wapya ni beki wa kati Mganda, Gift Fred kutoka SC Villa na Nickson Kibabage aliyekuwa akiitumikia Singida Big Stars sasa Singida Fountain Gate.

"Jana (juzi), tumemtambulisha 'Mbappe wa Congo', na amepewa jina hilo huko kwao kutokana na kiwango chake na spidi aliyonayo, tumepambana kwa kila njia kumpata, tumefanikiwa ni ongezeko zuri sana, wanachama na mashabiki wa Yanga watakuja 'kuinjoi' sana kwa mpira mzuri kutoka kwake," alisema Kamwe.

Aliongeza usajili huo umelenga kuendelea kuboresha kikosi na si kukitengeneza kwa sababu bado wana timu ambayo hakijaparaganyika.

INAENDELEA UK 23

# Ngoma rasmi mali ya Simba

## ●●● Wekundu wa Msimbazi sasa watangaza bado wapya wawili ambao...

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE kiungo mkabaji ambaye ni raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Fabrice Ngoma, ametambulishwa rasmi amejiunga na Simba akitokea kwa vigogo wa Sudan, Al Hilal.

Ulikuwa ni usajili unaosubiriwa kwa muda mrefu na wanachama na mashabiki wa Simba kutokana na kuwapo kwa tetesi za nyota huyo 'kutekwa' kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Julius Nyerere akiwa anatajwa yuko kwenye rada za kuwindwa na watani zao, Yanga na Azam FC.

Nyota huyo amekuwa jijini Dar es Salaam kwa muda wa wiki moja hapa nchini mpaka jana alipokamilisha mazungumzo ya kujiunga na Wekundu wa Msimbazi kwa ajili ya kuitumikia klabu hiyo kwenye mashindano mbalimbali katika msimu ujao.

Taarifa ya Simba imesema Ngoma ni mali ya klabu hiyo na ujio wake utaongeza nguvu katika kikosi chao na hatimaye kufikia malengo.

**Katika taarifa hiyo Simba imesema wamemnasa kiungo huyo baada ya kumnunua akitokea Al Hilal.**

"Tulimtaka na wengine walimtaka, lakini akachagua Simba," ilisema sehemu ya taarifa rasmi iliyotolewa na klabu hiyo.

Usajili wa Ngoma unaonekana unalenga kuongeza nguvu katika eneo la kiungo mkabaji kwa kushirikiana na Sadio Kanoute, raia wa Mali na Mtanzania Mzamiru Yassin.

Kabla ya kuingia mkataba na Simba, kiungo huyo wa zamani wa AS Vita Club na Raja Athletic Club ya Morocco, Al Hilal ilitangaza nia ya kumshtaki katika Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA) pamoja na wachezaji wenzake ililalamika wamevunja mikataba kwa kutofuata taratibu sahihi.

Simba ililazimika kufanya mazungumzo rasmi na Al Hilal na hatimaye kufikia makubaliano ya kumnunua Mkongomani huyo mwenye umri wa miaka 29.

Ngoma anaungana na Wlly Onana aliyetokea Rayon Sport ya Rwanda, Aubin Kramo Kouame (27) na beki wa kati, Che Fondoh Malone (24) aliyetua Msimbazi akitokea Cotonsport ya Cameroon.

Malone ametua Tanzania akitoka kutangazwa kuwa Mchezaji Bora wa Ligi Kuu Cameroon kwa msimu uliomalizika wa 2022/2023 huku akiwa muhimili muhimu kwenye kikosi cha timu ya Taifa Cameroon 'Indomitable Lions' kilichocheza michuano ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Kabla ya kuelekea nchini Uturuki kwa ajili ya kambi ya mazoezi, klabu hiyo ilimtangaza Mtanzania pekee ambaye amesajiliwa mpaka sasa, David Kameta 'Duchu', ambaye amerejea katika kikosi hicho baada ya kufanya vyema alipotolewa kwa mkopo.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema baada ya usajili huo kukamilika, bado wamebakiza wachezaji wawili ili kufunga mchakato wa usajili.

Ahmed alisema nafasi mojawapo katika usajili uliobakia ni ya golikipa na wanaka-

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002